Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

# MIONGOZO YA

## KIU

## KUFA KUZIKANA

## UTENGANO

**SIMON T KAWAIDA NA EDWIN ARIIHO**

**2019**

**MWANDISHI: MOHAMED S. MOHAMED**

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

**RIWAYA : KIU**

**MWAKA: 1970**

**UTANGULIZI**

Riwaya hii iliandikwa na Mohamed S. Mohamed mnamo mwaka 1970. Riwaya hii ilijipatia zawadi ya kwanza katika mashindano ya uandishi wa hadithi za kubuni katika lugha ya Kiswahili, ambayo yaliandaliwa mnamo mwaka 1970.

Mwandishi huyu, ametumia nadharia ya uhalisia katika utunzi wake wa kazi hii yaani, anazungumzia mambo yanayojitokeza katika jamii nyingi za dunia hasa za Afrika, kwamfano, anazungumzia juu ya usaliti wa namna yake kama Idi anavyomsaliti mzee mwingyi ambaye ni mwajiri wake lakini mwishowe anamsaliti kwa kumwoa Bahati ambaye mzee mwinyi anatamani sana na kumtuma Idi lakini yeye anasema kivyake. Isitoshe, mwandishi ametumiamandhari mbali mbali ili kujenga maudhui fulani fulani. Mandhari mingi yake hujikita sana Kwa Afrika kwa kuonyesha mienendo ya utamaduni, ndoa, Imani au itikadi ya miungu, maisha ya kawaida nk. Na haya yote huonyeshwa kutokana na uchoraji wa wahusika wake na mandhari na pia mbinu fulani fulani alizotumia.

**Fauku ya hay**o, mwandishi huzungumzia juu ya suala la mapenzi na athari yake, namna watu wanavyochukiana kwa ajili ya mapenzi na hasa mapenzi yasiyo ya dhati.

**Dhamira kuu:** Mwandishi analenga kuonyesha athari ya mapenzi yasiyo na msingi yaani mapenzi yasiyo ya dhati, kwamfano, mwandishi anamwonyesha Idi kama mlaghai wa mapenzi anayemlaghai Bahati ya kuwa yeye anampenda lakini yeye Idi hampendi ila tu anamtumia kama chombo cha starehe anataka kuitimiza shauku zake za kilimwengu.

Bahati anamwona Idi kama anayempenda bila kujua ya kuwa Idi ni chui anayejifunika kwa ngozi ya mbuzi. Baada ya miaka mitano kwa ndoa, Idi anaonyesha rangi yake kamili au kama vilivyo kuwa dhahiri shahiri yeye hampendi Bahati, sasa Bahati huanza kujuta kwani alijikuta ameishanaswa na kamba ya mapenzi lakini kamba isiyo ya ukweli labda ya ulaghai.

Vile vile mwandishi yataka **kuonyesha usaliti** ambao umejenga ghorofa kwa mioyo ya wanajamii husika. Mfano mzuri ni Idi ambaye anamsaliti mzee Mwinyi ambaye ni mwajiri wake anayemchukuwa kama ndugu yake, mtoto wake ingawa yeye ni mwajiriwa wake yaani ni dereva yake.

Mwinyi anamwamini sana Idi ndiyo sababu akimtuma kwa Bahati ili amwelezee ya kuwa anampenda lakini Idi anasema mambo yake na baadaye anamwoa yeye mwenyewe. Isitoshe, baada ya miaka mitano anatengana na Bahati na kuingia mapenzini na Rehema bintiye marehemu mzee Mwinyi.

**Sura ya kwanza (Uk 1-19)**

Mzee mwinyi kushikwa na kiu yaani kumpenda Bahati, bintiye Jaku na bibiye cheusi. Idi anampelekea ujumbe Bahati kuwa mzee Mwinyi anampenda na pia anamletea picha yake mzee Mwinyi anafurahi sana ndipo anajipiga moyo konde ili amnunulie nyumba kwa ajili ya mapenzi.

Mzee mwinyi na Idi kuelekea kwa Bahati kwa ajili ya mapenzi, barabara ilikuwa mbaya sana. Mwinyi anaanguka chini na kukumbatia ardhi….. Uk 4 na kusema **"Asemaye kuwa mapenzi ni laki ya kijanatu……."**

Kwa **Uk 11**, ndipo Idi anamwelezea mzee Mwinyi kuwa Bahati anafaa amnunulie nyumba kama zawadi yake ya kwanza kwa kumpenda.

Kwa **Uk 12**, idi yamsawisha Bahati ili ampende mzee Mwinyi kuwa ni mpango utakaowafanya wote wawili kutajirika- vile vile, **Uk 15**, anamwelezea kuwa wale wote waliotajirika, wote ni wizi…. Mwizi si Yule mtu anayevunja nyumba tu…..**mzee huyu utajiri wote ameupata wapi**?

**……… akajibualiurithi nani asiyejua kuwa babake alikuwa mwizi……?.**

Idi yataka kuingia mapenzini na Bahati lakini Bahati anamkataa wakati walipokwenda pamoja kutafuta nyumba , lakini Bahati yeye anaendelea kumkataa akisema **"mimi sina haja na mali ya mtu natosheka naumasikini wangu…..Uk16.**

Wote wako kwa Benzi, watoka kutafuta nyumba. Bahati anamtazama kwa mshangao mkubwa kwani sivyo alivyokuwa anamtarajia, sasa anaona vipi mambo yatakuwa….. **UK 16** akisema mimi sitaki. Sitaki hata kidogo……… mwishowe gari lake idi, likasimama kwao Bahati akashuka na Idi akamwambia kwa kejeli kuwa "**kwa heri ya milele …….Uk 19-19**, hakini njia ya kupitia sauti ilikuwa imefungwa ili aweze kumuomba msamaha lakini wapi? Alijikakamua kutaka kusema lakini yakatoka machozi badala ya sauti……**Uk 19**

**Sura ya pili: (Uk 19-47)**

Bahati kufika nyumbani baada ya kutoka kwa ziara yake naidi akafika nyumbani akighadhibika sana kwani anajiona kama ameacha bahati kwa kumkataa Idi kumpenda.

Cheusi anamwonya bintiye ili asiendelee na mapenzi na Idi wake akiapa akisema **"Baba yanguafufukekaburini".** Nenda uendako, fanya utakavyo, langu; litakuwa jicho tu!!! Lakini wapi! Hivyo sivyo ilivyo roho ya mzazi**……………….. Uk 26.**

Vile vile, baada ya siku tatu, Bahati ana shauku ya kuonana na Idi, akamwendea ……**Uk 30-31** ili aweze kumwomba msamaha amtafute kwani. Hakuweza kuishi bila Idi. Lakini hakujua

vile atakavyopokelewa,. Wakakutana na kufanya mapenzi pamoja na kuagana kuonana jioni hiyo**……Uk 34**.

Bahati yamgonjea Idi jioni hiyo na hakumwona, mpaka usiku anapokuja na mamake akimwona mlangoni akiufunga tena………. Halafu Bahati anakuja akitabasamu kidogo ingawa ameghadhibika kidogo kwasababu amemgonjea na hakumwona jioni kama walivyoahidiana.

Idi anamwelezea Bahati kuwa mzee mwinyi yu vibaya amekuwa hospitalini ndiyo sababu akavunja mradi wao, siku iliyofuata wakamtembelea mzee Mwinyi na akafurahi sana na kumpa hundi ya shillingi Bahati na halafu wakatoka. Vile vile mzee Mwinyi akamuuliza Idi, kuwa nyumba ile wakajinunua….Bahati ,Idi na Mwinyi wakakutana na kuzungumza mingi na halafu wakatoka **…….Uk 42**

Bahati akawa na ndoto nyingi sasa za kila rangi, aliota anaelekea Kongo kumtafuta baba yake. mara akaota akaingia mabegani mwa Idi, halafu akaota anapita madukani kutafuta vitamba vizuri na vitu vya anasa tupu……….. **Uk43**

Bahati na Idi wote watoka pamoja wako garini na wazungumza mafanikio yao, kutokana na zile pesa kutoka kwa mzee **Mwinyi Uk……47**, lakini Bahati bado ana wasi wasi, akasema ‘**haidhuru nitafanya kamautakavyonishauri…………Uk 47**.

<u>**Sura ya tatu (Uk 48 -62)**</u>

Mara tena Idi na Bahati wakamtembelea mzee Mwinyi, Mwinyi akafurahi sana, akamshika mkono Bahati kwa kitambo wakawa chumbani wao wawili na halafu wakatoka Idi akiwasubiri nje….. **Uk 48-49**

Baada ya kutoka kwa Mzee Mwinyi wanarejelea **Selea** wanakwenda kwa shauku ya mapenzi, ingawa Bahati juzi amegombana na mamake sasa anajifanya haidhuru kwani hakulala nyumbani jana…………sasa anajiuliza atamwambia suala gani mamake ili apate kutuliza hasira yake………………. **Uk 51**

**Uk 52,** punde si punde, mama mtu anamfokeam kali anataka amwelezee wazi pale anapotoka…….na Bahati husema **“Ah! Mama usinikaripie katika saa yangu ya mwisho nipe buriani yako**, **nife kwasalama……… UK 53 utakufa? Duniani nitakaa na nani? ………baba yako kanikimbia……….**

**Uk 54,** Idi anamfanyia utani Mwinyi mara alipomrudia kuona hali yake na kukuta hali yake kazidi kuwa mbaya akasema njia moja tu bwana **Mwinyi ni kumwoa Yule binti na kuishi pamoja …………. Uk 54.** Akamshauri kuwa asimwambie kuwa yataka kumwoa ila tu

matendoyake yatamfanya Bahati mwenyewe kukubali, kwani ndio mwenendo wa wasichana wa siku hizi………………

Mara nyingine Bahati alipomwendea Mwinyi walimaliza muda mrefu wawili wakizungumza Idi akiwagonjea nje na halafu wakarudi Selea na kusemeana kuwa mtego wao umefika kileleni. Baadaye Bahati anampa hundi ya shilingi kabla hajarudi kwake Idi wakati anapomfikisha kwao **Uk 57.**

**Baada ya siku nne** kutoka kwa ziara yao kwa mzee Mwinyi, Idi alianza kuwazia utajiri ambao amepata kutoka kwake akaona kuwa zilikuwa pesa nyingisana………………**Uk 58**.

Bahati kumwandikia barua ya utani Idi eti "

***Idi, usistaajabu nikikwambia ya kuwa hisa sasa niko kitandani kwa Bwana mwinyi tunapanga siku ya arusi yetu ya kikweli si ruhusa kutuingilia kwani tuna hiari yetu. Nakuonya kwa salama yako mwenyewe, kuwa mipango iwe imekoma baada ya kuipata barua hii. Nisalamie Fulani………………***

***Wa nafsi yangu,***

***Bahati***"

Barua hii ilimchemsha moto Idi moyoni mwake ilimwia dhomba kali ya ghafla ………… **Uk 58-59**

Baadaye, Bahati anakutana na Idi ana kwa ana anajifanya kama hana habari yeyote na mwishowe akamwelezea Idi eti ulikuwa utani tu…………….na halafu wakazungumza juu ya mipango ya ndoa yao. Ujenzi wa nyumba yao ya ghorofa ……… Bahati akasema nakupenda Idi wangu …………naye vile Idi akasema usininyime arusi yako na mwinyi" …………uk.62

**<u>Sura ya nne (Uk 62-72)</u>**

Kila jioni Bahati na Idi wangekutana na kuzungumza ujao wao, Bahati zile huruma ambazo angemwonesha mamake zikageuka mvuke katika joto la mapenzi zikapotea alichokiona kina maana zaidi kwake kilikuwa matembezi yake kwa Idi …………**Uk 63**

Mzee Mwinyi aliendelea kutoa mifedha maelfu na maelfu kumpelekea Bahati ingawa maisha yake taabani yameendelea kuwa kitendawili.

**Idi anamwelezea kuwa kule anapokaa hiyo si nyumba labda ni kibanda cha kuku na Bahati akisema "Ah, mimi sina wasiwasi nichukue popote mradi nitakalo mimi ni kuishi pamoja na wewe tu …… Uk 65**

Bahati kutembelea, marafiki zake wa zamani akina, kidawa na Tatu lakini anakuta wote wanaishi katika maisha ya vuta ni kuvute hawana raha kama ile anayotarajia kwa ndoa, lakini Bahati anajiwazia eti labda walifanya chaguo baya lakini mimi na idi wangu **chaguo baya lakini mimi naIdi wangu ……..kifo tu ndioutengano wetu……………. Uk 67**

**<u>Sura ya Tano (Uk 72-Uk 84)I</u>**

Idi kwenda selea kwa mamake Bahati-cheusi kuleta posa. Cheusi akamfurahia na Idi kutaka ndoa yao ya kirasmi itendekwe mnano wa wiki moja………… mama- mtu anawapa Baraka ili waweze kuishi kwa amani na nguvu kama bibi na bwana **…………………..Uk 73**.

Harakati za arusi zika anza, chesi akawaita watu kufanya matayarisho kama; Bimvita Biti songoro, Hadija………..Cheusi alishangaa sana na zile notiza pesa alizopewa kwa ajili ya maandilizi ya karamu hiypo **………….Uk 73.**

Karamu ikafana sana na vile, sherehe yao ikafanywa kiutamaduni ambapo, shehe aliarikwa ili aje akawafanyie shughuli fulani kuwaunganisha kama Bibi na bwana, Shehe Baraka alikalia mkeka akpeleka mkono kwenye saa yake yenye mkufu wa fedha, ambayo siku za mavuno kama hii huzekebisha mapema**……….. Uk 84**.

Karamu ikafana sana watu wakalana wakafurahi sana ndipo wakaanza kucheza akina Biti Jaku, Hadija na Cheusi na kustani . mirindimo ya msondo ikavuma hata kuta za kijumba kile zikavuma na kuwa sehemu ya ngoma…………. **Uk** 82-83

Vile vile Hadija akamwiimbia Bahati anapojizoazoa kitandani eti

> **Mwana aingilie chooni**
>
> **Aingie koga marashi**
>
> **Uvumba na ndi………..**

Sauti zikachangamyika na wote wakaimba

> **Mwana aingilie chooni,**
>
> **Aingie koga marashi**
>
> **Uvumba na udi…………………Uk 83**

<u>Sura ya sita (uk 85-Uk 94)</u>

Hali ya mzee mwinyi kuendelea kuwa vibaya na Idi tokea tangu aanze shughuli za kujenga nyumba yake ya ghorofa na mikakati ya ndoa hajarudi kwake ingawa ana gari lake. Mwajuma naye anaona kimya hiki kuwa si kimya cha uzima labda kuna jambo jingine-

Mwanajuma anampa ufadhili mzee mwinyi lakini hasemi neno, ndipo mwajuma akamuuliza "ni nani? Bahati ambaye hutamka kila wakati usingizini lakini hakumwambia…………Uk 87.

Kwa Uk 87, mzee mwinyi akasikia sauti ya ngurumo ya Benzi yake……. Uk 87.

Lakini Idi akaileta nakuiegesha pahala pake na vifunguo lakini hakumsalimu mzee na hata mwajuma.

Mwinyi anaendelea kulia kwa kiu ya mapenzi kwa Bahati anaanguka chini mwajuma anamkuta chini macho akiyakodelea dirishani akamuuliza yataka nini lakini hasemi…….. Uk 89, kuona kwa egesho la magari akaikuta ile Benzi lakini hamwoni Idi aliyejileta ……………… na kujiuliza maswali mengi.

Kwa **Uk 90-91,** mganga anakuja, kumtibu na kuuliza wapi Idi yuko? Lakini mwajuma hana neon hata kidogo . Baada ya kitambo tu, mzee mwinyi akakata roho……………..**Uk 91.**

Mwajuma, akaenda kwa Idi-Buraha lakini anapomwelezea habari juu ya kifo cha mzee mwinyi, mara **moja Idi akamwelezea nenda ukamzike**……..huo ni wakati, Idi na Bahati wako katika siku zao za kwanza ndoani.

Mwajuma akapiga ripoti kwa polisi na mzee mwinyi wakamzika kama mtu asiyekuwa na wa kwao kwani Bintiye Rehema yuko ulaya ndipo anaposomea…………**Uk 94**. Vile akazikwa nachama cha **" umoja wakuzikana**"

**Sura ya saba (Uk 94-116)**

Miaka mitano imepitaya Idi na Bahati katika ndoa yao lakini sasa kuna mabadiliko makubwa………Bahati akanyaona mangapi?........akayasikia mangapi? ……….Uk 95 kiu**……..ahi, kiu ndiyo kila siku, kila kitu kiu imeumbwa pamoja na uhai, itaondoka na pamoja na uhai…………..**

Bahati anaanza kujuta akisema afadhali aishi katika umaskini wake kuliko kuishi katika utajiri wenye matata kama anayokutana nayo sasa. Bwanake amegeuka, mlevi, nyumbani halali, akija fujo tele.

Bahati kumtembelea Yule mvuvi Yule wa Bahari na kuzungumza naye kwa muda mrefu nakusema afadhali maisha yake kuliko maisha yale ya kifahari ambayo kwake sasa hayana maana……….**Uk 103.**

**Kwa Uk 111**, Bahati akaanza kujiwazia Id ialivyokuja nakumrambishana mapenzi akamhidi kasiki nzima………. Alikuwa na kiu ya mapenzi, mapenzi aliyoahadiwa. Lakini badala ya

mapenzi ndiyo alipata unyonge na yule aliyemwahidi, mshirika wake sasa amepata wengine na sasa si mmoja wao…………

**Kwa Uk 115**, Bahati anapata majeraha wakati anapotaka kumchukua Bwanake-Idi mlevi sasa lakini anapojajribu kumchukua waanguka chini sasa Bahati ndiye anayejeruhiwa vibaya.

**Sura ya nane (Uk 116-150)**

Bahati kulazwa hospitalini kwa ajili ya majeraha aliyopata wakati anapotaka kumpeleka Bwanake mlevi….. sasa anaanza kujiambia eti yeye si kitu kwa Idi, yaani hayuko moyoni mwake kwasababu kwa siku kadha Idi hasi kumwona hospitalini**…. Uk 117**, Anapokuja anampitapitia tu, hakuna la maana alilomfanyia. Bahati akawa na biwi la moto ndani ya moyo wake la mapenzi likitoa ndimi kiu ya Idi…….. **Uk 119**. huku machozi yakimtoka

Shoga wake wa zamani akina **kidawa** na Tatu wakaja hospitalini kumwona na kumsihi kuwa **Dunia ndivyo hivyo…… Uk 120**

**Kwa Uk 121, Uk 122**, Bahati anarudi nyumbani na nyumbani anakuta mpishi aliyeacha nyumbani hayuko. Sasa kuna mpya ambaye nimwajuma aliyekuwa mpishi wa mzee mwinyi. Bahati mwanzoni alimhofu lakini baadaye wakafikiana wakawa wapenzi wakitembea pamoja na kuzungumza hadithi ziwahusuao……

**Kwa Uk 128,** mwajuma na Bahati watembea kidogo kidogo ili aweze kufanyia mazoezi mguu wake.

Kwa **Uk 134**, Bahati anashika mkono mwajuma kama "**mfa kiu aombavyo maji** ili amwelezee habari iliyotokea wakati alipokuwa hospitalini………….

Mwajuma akamwambia kila kitu na akamshauri aombe ruhusa kama anayekwenda kwao na halafu arudi jioni hiyo hiyo…… akafanya hivyo hivyo ndipo Bahati kumkutaIdi bwanake ana kwa ana naRehema bintiye mzee mwinyina Idi kumtusi Bahati akimwiita paka wa nyumba wakati Rehema yaani Malaya wake anapomuuliza kuwa yeye ni nai anayewavamia….. Uk 148

Bahati akaanza kusimulia hadithi namna Idi alivyokuja kwake kumwambia namna Yule mzee mwinyi alivyokuwa akimpenda na pia akamwambia kuwa akili zake hazimtoshi sasa akamtaka yeye washirikiane…………. Wandanganye ……………Uk 139

Vile vile akakumbuka maneno ya mama ya kumkatisha Idi wake ndipo anakumbuka kumkatisha idi wake ndipo anakumbuka kuwa "**sikio la kufa halisikii dawa"**

**Sura ya tisa (Uk 150 – Uk 158) (Utengano waBahati na idi)**

Sasa ndoa yao hayendeki mbele mara nyingine. Ikasitawi kwa miaka mitano tu, Bahati akarudi kwao **selea**, mama akampokea na kumtuliza.

**Fauku ya hayo**, mwajuma anamtembelea kumwelezea mambo yalivyo huko Buraha Idi na Rehema –Malaya wake.

Cheusi anamwapia mtotowe, kwa amepata habari kuwa Jaku yaani Babake wamepata habari kuwa alikuwa kongo na wakati wowote atakuja, sasa wote wana kiu ya kuonana naye tena.

Bahati anamwandikia barua Idi akidai baadhi ya mali na baadaye anamwita ili aje waonane, lakini mwisho Bahati harudi nyumbani mama anamtafuta hapa na pale lakini bure**……..UK 158**

**Maudhui yaliyomo**

(i)**Mapenzi**: Riwaya nzima imejengwa juu ya mapenzi kwamfano, mzee mwinyi ana shauku kubwa ya mapenzi kwa Bahati, ndiyo maana anamminia hundi za shilingi kwa ajili ya mapenzi.

**Isitoshe**: Idi anapendana na Bahati kwa ndoa yao ingawa mwishowe mambo hubadilika kwani Idi anageuka kuwa msherati, mlevi na, mapenzi yao yakawa kitendawili.

**Vilevile:**Bahati anapendana na mamake cheusi ndiyo maana wakati mamake anahagaika, Bahati alipotoka nyumbani kighafla bila kumwelezea.

(ii) **Usaliti**: Hujitokeza kwa Riwaya hii na hujidhihirishwa na idi ambaye anamsaliti mzee mwinyi. Mwinyi ni mwajiri wake yaani Idi ni dereva yake, mwinyi anamchukua kama ndugu au mtoto wake lakini mwishowe anamsaliti kwa kumwiibia pesa zake. Yeye na Bahati kumdanganya eti anampenda na kumpa pesa nyingi mno. Isitoshe, Idi anakataa kwenda kumwona mzee huyo wakati anapoungua vibaya na hata kukataa kumzika kweli kweli huo ni usaliti mkubwa.

(iii) **Utamaduni**: Kuna itikadi na uaminifu wa mila na desturi katika Riwaya hii, yaani mikakati na mipango yote ya arusi ya Idi na Bahati inafanywa kutegemea mila na desturi zao kwani, shehe anaitwa ili kuongoza sherehe hiyo kwa kuwaombea hawa wawili ili waweze kuwa bibi na bwana wa daima dawamu.

Vile vile. Bi mvita na Hadifja qwaanza kumrai rai Bahati Harusi na kumwiimbia wimbo wa kiutamaduni eti “**mwan aingilie chooni**

**Aingilie koga marashi**

**Uvumba na udi….. Uk 83**

**(iv) Utajiri** : Katika Riwaya hii kuna maudhui ya utajiri yanayojidhihirishwa kwamfano mzee mwinyi ni tajiri kwani anaajiri watu kama Idi, mwajuma na vile vile ana magari kama Benz, mtoto wake wa kike anasomea ughaibuni . Rehema **pengine**, Idi mwenyewe ni tajiri kwani anajenga nyumba ya ghorofa huko Buraha na ana watumishi mbalimbali. Jambo linguine wakati Idi anapomsawisha Bahati akimwelezea eti ile nyumba yake ilikuwa kibanda cha kuku akiamhidi kuwa atamjengeanyuimba ya ghorafa.

**(v) Umasikini:** vile vile kuna maudhini ya umasikini kwamfano Bahati kwao selea ni masikini kwani nyumba yao imezeeka sana-imemaliza miaka nyingi bila kufanyiwa marekebesho yaani kupigwa chokaa **vilevile**Idi anamwambia eti hajachoka kula chakula cha aina moja yaani kwake wanakula kuku nk kila siku kama kwao wanavyokula maharage. Hayo yote ni ishara kuwa kuna umasikini mkubwa.

**(iv) Umoja**: Kuna umoja katika Riwaya hii kwamfano wakati wanapoandaa arusi ya Bahati na Idi waandalizi kama; **Hadija, Bi.Mvita, Cheusi, B.songoro** waonyesha ushirikiano na umoja wa aina ya juu katika harakati zenyewe.

Pia, **cheusi** anashirikiana sana na bintiye katika kazi za nyumbani kama upishi nk.

**(vii) Utengano**: Kwa utengano katika Riwaya hii, kwamfano utengano kati ya mzee mwinyi na Idi, baada ya idi kamwoa Bahati ambaye mwinyi amepata kiu na Yule aliyekuwa akituma ndiye anayemsaliti na baadaye wakatengana.

**Peng**ine, utengano kati ya Idi na Bahati baada ya miaka mitano ndoani mwao.

**Isitoshe**, utengano kati yaJaku na familia yake yaani amemaliza miaka kumi na nane kutoka wakati alipotoka nyumbani na wanafamilia hawajui wapi alipokwenda.

Mzee mwinyi akatengana nadunia baada ya kifo chake.

(**viii) Ulevi**: kuna ulevi katika Riwaya hii kwamfano Idi ni mlevi yaani kila siku anakuja nyumbani akiwa ameleveka sana na mwenye maneno yenye matusi kwa bibiye Bahati.

**(ix) Urafiki:** Kuna kupendana kwamfano; Bahati anapendana na kidawa na Tatu marafiki zake wa zamani yaani wanatembeleana na kutolea habari fulani fulani.

(**x**) **Uvivu**: Kuna maudhui ya uvivu kwamfano cheusi anapokwenda kwa mponda ili aweze kumwazima nyumba yake kwa ajili ya wageni wake lakini mkewe akakataa…… Uk 76

**(xi) Kiu**: Riwaya yenyewe, mwandishi ametumia kiu kama taswira yaani mbinu mojawapo kuwasilisha kuwa na shauku kwa kitu Fulani kwamfano; mwinyi ana kiu kwa mapenzi kwa

Bahati, bahati naye vile anaonyesha shauku nakiu kwaIdi ili aweze kumwoa kama bibiye lakini baada ya miaka mitano hana raha naye tena yotebaina yaoyamekwisha …….Uk 157.

(**Xii)Unyanyashaji:** Katika Riwaya hii kuna maudhui ya unyanyashaji kwamfano kulingana na kidawa na Tatu wanavyolia wakinyesha namna mabwana zao wanavyowanyanyasha wakirudi nyumbani wakiwa wameeleveka na pengine Bahati naye vile ananyanyashwa na Idi na kutusiwa kwa kumwiita paka mbeleni mwa Malaya wake.

**(xiii) Uhawara/ umalaya:** Mfano dhahiri ni wa Idi yaani ni msherati kwani anaingia mapenzini na Bahati kwa kumdanganya kutoka kwa mzee mwinyi mwajiri wake. Vile vile hujitokeza kulingana na maneno yaBahati akidai kuwa bwanake ni mlevi na hatamsherati nahatawakati anapomkuta ana kwa ana na Malaya wake-Rehema na kumtusi kwa kumwita paka……… **Uk 151 & 152**

**(xiv) Uvumilivu**

**Mbinu za mwandishi**

Mbinu za mwandishi mara nyingi huitwa fani za mwandishi, na zile njia mwandishi anazotumia kuwakilisha ujumbe wake kwa jamii hudiks. Mwandishi yaweza kutumia mbinu tofauti tofati kama Mohamed S Mohamed aliyotumia

**Taswira**: ni kujenga picha Fulani katika akili ya msomaji au mtazamaji. Kwamfano, katika Riwaya hii MWANDISHI ametumia neno “kiu” kuonyesha shauku ya kitu Fulani, yaani msomaji anaweza kufikiria **juu ya kiu na kusema kiu ni kitu gani**………………… mzee mwinyi anakufa kwasababu ya kiu,Bahati anaolewa na idi kwasababu ya kiu kwa hivyo, mwandishi amefanikisha kaziye kwa kutumia mbinu hii.

**Jazanda/istiari**: ni ulinganishi wa moja kwa moja kwa kutumia neno kama, sawa sawa na, pamoja na, kama na mithili ya………………. Kwamfano mwajuma anaposema **eti “mawe”! Moyo wa mwanamume sawasawa na ndege akitutoka humwoni tena ……………….Uk 136. Uk 134 Bahati akizungumza** juu ya kiu ya bwanake akisema …………………….kama mfa...- kiu aombavyo maji……………….niyambie mwajuma **…………….Uk 134.**

**Nyimbo:** Mwandishi ametumia mbinu ya nyimbo ili kuwasilisha ujumbe Fulani Fulani. Kwamfano **Uk 83** Hadija na wengine wanamwiimbia Bahati wimbo wa kiutamaduni wakati wake wa kuolewa . wimbo huo unadhihirisha utamaduni wao kikamilifu.

**Barua :** vile vile mbinu ya barua imetumiwa katika Riwaya hii kwamfano kwa **Uk 58-59**,, Bahati anapomwandikia barua kumujulisha kuwa yeye na mzee mwinyi wako tiyari kupigana ndoa. Ingawa ujumbe kamili uliokuwepo ulikuwa wa dhihaka au tabaini au tuseme kinaya.

**Isitoshe:** Idi anamwandikia barua **Bahati Uk 157**, akimwelezea ili aje wakutane baada ya kutengana kwa muda.

**Kuboranga lugha**: Kutumia lugha isiyo saluti kisarufi kwamfano **Uk 71**

**Takiriri**: Ni mbinu ya kurudiarudia maneno ili kusisitiza jambo Fulani kwamfano; Uk 148, toka….toka….toka!! wakati **Bahati anapokuja nyumbani na kumkuta Bwanake na malaya na kumfukuza hivyo hivyo. Pengine Bahati akaanguka chini akalia …………..akalia…..akalia**………kitambo.

**Methali**: Ni maneno au fungu ya maneno yenye maana fiche, kwamfano**; Uk 140 sikio la kufa halisikiidawa, wakati** Bahati anapo kumbuka namna mamake alivyomshauri shauri. Unifae la jua nikufuae la **mvua – wakati cheusi anapo kwenda kwa salama ili amzime na chumba ili awakaribishe wageni wake Uk 76 na vile Uk 75, siku njema huonekana asubuhi wakati cheusi** anapotayarisha kupokea wageni wake akiona mambo yakienda sambamba.

**Usimulizi** Mwandishi ametumia mbinu ya usimulizi yaani kusimulia kisha fulani kitabuni kwa mfano **Uk 139** , Bahati anaposimulia hadithi namna Idi alipokuja kwake mara yake ya kwanza kumwambia kuwa mwinyi anavyompenda lakini baadaye anageuza maneno yake kuwa ndiye anayempanda na Bahati kusitasita kidogo lakini baadaye akawa na kiu na mapenzi kwake.

**Msemo**: kwamfano Uk 76, kupata si kukosa, akkajua fedhela iko njiani ni wakaticheusi anapohangaika akitafuta chumba cha kukribisha wageni wake.

**Tahakuki** : Mwandishi ametumia mbinu ya Taharuki kwamfano hatujui iwapo Jaku alirudi nyumbani au la?

**Vilevile**: Hatujui Bahati aliishia wapi tokea wakati anapokwenda kukutana na Idi kuhusu suala la kugawanya mali yao baada ya utengano

**Lugha mseto/kuchanganya ndimi**, kwa mfano **Uk 148,** Rehema anaposemana ni Yule darl………….

Jazanda/isitiari: Kutumia **neno"kama" au "mithili ya " kwa mfano,** Bahati akageuka kama sanamu. Uk 148, maara aliushika mkono na kumwomba, kama mfa kiu aombabyo maji….. Uk 134

- Mbinu nyingine kama;

- Dhihaka /**tabaini Uk 58** barua yenyewe
- **Swali la balagha Uk 85.**
- ***Majibizano Uk 133, 134***
- ***Mdokezo wa maneno .***
- ***Alama za mshangao***

Pengine , mwandishi ametumia mbinu ya kinaya. Kwamfano, Idi anamsawisha Bahati eti anampenda lakini baada ya miaka mitano mapenzi hayo hayako tena.

Vilevile: Idi aliyekuwa rafiki wa ndani na mzee mwinyi anamtendea matendo ya kinaya kwa kumwoa bahati kipenzi chake.

**Tawasifu/hulka/wasifu/sifa za wahusika**

Mwandishi wa Riwaya hii ameunda wahusika wake na kuwapa hulka mbali mbali ambazo husimamia pakubwa kwa ujenzi wa maudhui yake.

Mtunzi kwa kufanya hayo, yataka kuitimiza lengo/dhamira yake;

Mhusika mwinyi huangaliwa kama Tajiri kwani ana gari la aina ya Benz, mtoto wake Rehema husomea ughaibuni –ulaya, ana wafanyikazi nyumbani kama, huangalia kama mwenye mapenzi kwani anapatakiu ya mapenzi kwa huyu binti mdogo-Bahati

Pengine huangalia kama mwenye utu kwani humchukua Idi kama nduguye ingawa ni mfanyikazi wake na mwishowe anamsaliti.

**<u>Idi</u>**: Huangaliwa kama msaliti mkubwa aribaye hawezi akaishi kwa manenoyake kwamfano, anamdanganya Bahati eti anampenda na baada ya mwaka mitano anamtupilia mbali.

**<u>Pengine</u>**: yeye ni minyanganyi kwani anamnyanganya mzee mwinyi pesa zake akijizatiti kuwa kuinganishi kati yake na Bahati lakini baadaye anajisemea maneno yake.

**<u>Fauku ya hayo</u>**: Idi ni ulevi, mnyanyashaji na hata mwenye matusi anayemtusi mkewe kila wakati akija nyumbani usiku, pia wakati anapomleta Malaya wakae nyumbani na kukutana ana kwa ana na Bahati na kumwiita mkewe paka wa nyumbani.

**<u>Pia</u>**: Idi ni mwenye kichwa kigumu na hata anajigamba, anajiona bora kulingana na maneno Bahati eti "nikikuona kama bibi yangu nitakujengea nyumba ya ghorafa huko Buraha kwani hii si nyumba labda kibanda cha kuku….." pia anapomwelezea kuwa hajachoka nachakula cha aina moja…… kwani kwao wanakula kuku nk kama kwao wanavyokula maharage.

**<u>Isitoshe:</u>** Idi ni mwenye lugha ya kejeli kwani, Bahati anapokwenda kumtembelea mara yake ya kwanza anasema "**nilijua utajileta**: na Bahati akaishiwa na maneno.

**Bahati**: Ni mwenye mapenzi yaani, anapopendana na Idi anakosa hata kula ingawa mamake anamshauri na hata kuapa kuwa bwanake hampendi, Bahati anaona mamake kama anamchukia. Vilevile, anapendana na mamakekwa kuwa na ushirikiano naye nyumbani na kufanya pamoja kazi za kinyumbani.

**Pengine**: Ni mwnye mapenzi, anapendana na marafiki zake kama kidawa, Tatu na hata mwajuma yaani wanasikilizana na hata wanatembeleana.

**Isitoshe**: Bahati ni mvumilivu ambaye anamuilia ulevi na uasherati wa bwanake na pia matusi yake kwa ujumla.

**Vilevile,** Bahati ni mwenye kichwa kigumu kwani ingawa mamake anakanusha jambo lake la mapenzi na Idi lakini yeye anaendelea naye.

**Pia**: Bahati ni mdangariyifu kwani yeye na Idi wanaudanganya mzee mwinyi pesa zake ingawa hampendi.Cheusi: Ni mamake Bahati, mkewe Jaku aliyepotelea kongo kwa miaka tele, ni mwenye huruma kwani anamhurumia motto wake anapopata mizozo na bwanake Idi.

**Vilevile:** Ni Mwenye ushauri yaaani anamushauri bintiye asiendelee mapenzini na Idi kwani ameishatambua kwa Idi hampendi lakini Bahati anendelea naye.

**Pia** : Ni mwenye juhudi kwamfano, wakati wa matayarisho wa karamu ya Bahati na Idi yuko juu chini ili kuona ya kuwa karamu hiyo ni "fanikio"

**Cheusi pia**: huangaliwa kama mwenye bidii kwani anatia bidii nyingi akifanya, kazi kama za kuuza vitumbua maandazi nk ili kujipatia riziki.

**Vilevile,** ni mvumilivu yaani anavumilia na kazi zote za nyumbani akiwa na matumaini kuwa labda siku moja bwanake Jaku atarudi nyumbani baada ya miaka kadhaa bila kurudi nyumbani.

**Mwajuma**: Ni mtumishi wamzee mwinyi ambaye ni mwenye juhudi kwani anfanya kazi yake bila kizuizi chochote.

***Pia***: ni mwenye mapenzi na mficha siri kwani anamfichulia siri Bahati kuwa bwanake ni msherati hata ana mshauri ili aende kwa Idi kudai mali yake baada ya utengano wao.

**Rehema**: Ni bintiye mzee mwinyi, ni msomi yaani anasomea ughaibuni –ulaya, ni Malaya kwani anamvamia Bahati ndoani yake na mwenye matusi kulingana na kile viliyotokea Bahati anapowakuta ana kwa ana.

**Jaku**: Ni babake Bahati, bwanake cheusi aliyekwenda kutoka nyumbani bila kuwaambia wanafamilia wapi amekwenda, na kumaliza miaka kadhaa.

**Mkewe mponda**: Ni mwenye uvivu kwani cheusi anapokwenda kwao ili waweze kumwazimia na chumba ili aweze kupokea wageni wake anamwonea na chuki na wivu mkali wahusika wengine kama, Bi.songoro, sala, Bi.mvita na Hadija huonyesha sifa ya umoja wakatiwanpoanda karamu ya Bahati na Idi.

**Vilevile:** Huanyesha sifa ya kuwa wanautamaduni wanapomwiimbia wimbo Bahati anapokwenda kuolewa.

**RIWAYA : KUFA KUZIKANA**

**MWANDISHI: KEN WALIBORA**

**MWAKA: 2006**

**Utangulizi:** Riwaya hii iliandikwa na Ken walibora mwaka wa 2003 na kuchapishwa mara ya kwanza 2006.
**Kufa kuzikana** ni hadithi ya urafiki kati ya vijana wawili , Akida na Tim, wanaotoka kwenye makabila yenye uadui. Ni hadithi ya migogoro, mingongano, vikwazo na vizingiti katika uhusiano wao. Je, urafiki wao huo unaweza kuvistahimili vishindo hivyo? Je ni urafiki wa kinafiki au una nguvu ambazo hazishindiki?

Riwaya yenyewe huzungumzia maswala **ya kiuhalisia yaani ;**
**Ukabila na utamaduni,** maadili na mapenzi, usawa wa kijinsia na uhuru wa mtu binafsi. Hayo yote hujidhihirishwa na hulka/tawasifu au namna mwandishi alivyochora wahusika wake na kuwapa majukumu mbali mbali.

**Dhamira ya mtunzi** : mtunzi katika Riwaya hii analenga kuonyesha athari mbaya wa ukabila yaani anaonesha ukabila kati ya makundi mawili yaani wakanju na wakorosho wanavyo chukiana, wanavyouana, wanavyotusiana kwamfano katika **Uk 26** ambapo Akida

na Tim wanapo mtembelea mjombake Tim na kusema eti ***Hakuna mkanju ana mke mmoja, wakanju wanapenda matanga sijui matanga ya mjomba, sijui matanga ya binamu ……… wataanzahata kuenda matanga ya mbwa nap aka…***

Hayo yote yajitokeza wakati mjombake Tim anapomwuliza kuwa babake ana wanawake wangapi?

Kweli kweli, ukabila katika nchi ya kiwachema umejenga ghorofa katika mioyo ya wananchi hii na wengi wao waameathiriwa vibaya kama kupoteza nafasi serikali, kupoteza maisha na kuongeza chuki nchini nzima.

**Vile vile** ; **mwandishi yataka kuonyesha urafiki wa dhati au kufa kuzikana ingawa ni wa kabila tofauti tofauti yaani Akida ni mkanju na Tim ni mkorosho lakini** wanakutania shuleni na wapendana, nyumbani wanachukiana wanauna katika vita vya kikabila na kwa hivyo, mwandishi anataka kuonyesha dhima ya urafiki hata urafiki wa dhati au wa ukweli ambao unakumbwa na vizingiti au vikwazo mbali mbali lakini wao wakendelea daima dawamu.

**Mandhari:** Riwaya hii mandhari yake ni kiafrika hasa hasa nchini Kenya kwani mahali mengi yanayozungumziwa yanahusiana sana kama:- kiwachema, sangura. Vile vile mandhari yake ni ya kiafrika kwani maudhui mengi yanayojengwa yanahusu sana mambo yanayokumba nchi za kiafrika kama;- **ukoloni mamboleo, usaliti, ukabila nk.**

**Pengine : Riwaya hii, kiwakati ni ya kisasa kwani inazungumzia mambo ya kisasa** ; elimu, urafiki wa kisasa na mitazamo mipya kuhusu ukabila kulingana na uchoraji na maudhui husika na utendaji wake.

**Jalada**: mwandishi ametumia picha mbali mbali yaani wahukika wawili wanonyesha nyuso zenye huzuni na machozi yakitiririka, ishara kuwa kuna mambo ambayo hayaendi vizuri.

**Pengine**: Jina lake "Ken Walibora" limeandikwa kwa rangi nyekundu ishara kuwa kuna matatizo mengi yanayosheheni Riwaya nzima.

**Isitoshe:** kwa jalada/gamba lenyewe kuna vibanda ambavyo vimechomeka na moto na kuna mbwa ambaye anatafuna kitu Fulani labda yaweza kuwa mifupa ya watu ambao wananauawa kwa vita vya kikabila.

**Uchambuzi wa Riwaya yenyewe kwa ujumla (ploti)**

Riwaya yenyewe huanza na mhusika Akida akienda mjini- kiwachema ili aweze kuzawadiwa na wizara ya elimu baada ya kuwa miongoni mwa wanafunzi waliofanya vizuri katika mitihani ya kitaifa yaani akawa mtu wa tatu nchini kiwachema.

Uko1 , Akida wanapofika, Tungule anakumbuka kifo cha mamake aliyefariki katika ajali walipokuwa wakienda huko mjini.

Vile vile, Akida anaenda mjini ili apate kujua mswada wa babake umefika wapi yaani babake yu mgonjwa na ana matumaini mingi kuona mswada wake ukichapishwa.

Akida anakumbuka mwalimu wake Alex aliyekuwa mkorosho kama Tim mtegemezi wake jijini ingawa wakorosho wengi hawakumpenda kwasababu alikuwa na ushirikiano mkubwa na wakanju.

Anakumbuka manemo ya mbunge Jonhstone mabende katika kituo cha biashara cha Baraki akiwatusi wakanju akisema ***" Hatutaki madoadoa, wakanju wahame waende kwao kanju……… Uk 02.***

Akida na wenzake kwenda kwa mzee mangala ambaye ni mmoja wao watu wachache wenye redio kijijini ili waweze kusikiliza matangazo ya mpira ….Uk 03. Kwani Timu ya taifa ya kiwachema ILIKUWA INACHUANA NA Timu ya Kenya na mambo ya ukabila yakaibuka sana wakisema wale wachezaji ni wakorosho yaani Timu ya Taifa haiwezi kukamulika bila wao………………………. Uk 04

Kuuawa kwa mwalimu Alex, na wakorosho kudai kuwa wakanju ndio waliomuua na kudai kuwa wahamie kwao kanju na ishara ya vita vya kikabila zikaonekana sana…….**uk 6**

**Sura ya pili**

Akida kufika jijini Tandika **uk 07**, mara yake ya kwanza na kwa mshangao mkubwa.

Anamtegemea sana Tim, mkorosho biniye mzee Zablon, aliyemsasidia kutokana na wachokozi shuleni….. Uk 08, kutokana na hayo wakaanza kuitana "shemeji" ingawa ni jambo la nadra sana mkanju kumwoa mkorosho….. Jambo jingine Akida hakubahatika nadada yeyote ………………**Uk 8.**

Tim akawa Rafiki yake wa kufa kuzikana nap engine alioea sana kuja kwao kusuhudia kipawa cha babake mzee sululu mwenye kipawa cha utunzi nyimbo na ala hizo**…. Uk 08.**

TIM akawa Rafiki yake wa kufa kuzikana na pengine alizoea sana kuja kwao kusuhudia kipawa cha babake mzee sululu mwenye kipawa cha utunzi nyimbo na ola hizo……….Uk08

**Isitoshe**, anapenda sana kutokan na siku ile alipomponya kutokana na janga la kuumwa na nyoka alipokuwa bado mtoto mdogo**…………………Uk 09**

Jambo la kwenda Jijini Tandika ni jambo ambao linahusiana sana na watu wanaokwenda kwa mahakama kwa ajili ya keshi zao au labda kwenda kwa hospitali kuu ya Rufaa Jijini..**Uk09**

Babake Akida kumwambia ili aende kwa Bwana **Gembo apate kujua madai ya malipo ya bima ya hayati mamake. Pengine aende kwa hatubagui publishers…………….uk 11**

**Uk 11**, kwa ukunjufu na Bashasha, tim anampokea shemeji yake…… wakaenda mkahawani wakala na wakanywa na Akida akashangaa kwa chakula walichowaletea kwani yeye alizoea na vyakula vya kijiji siyo **chips na sauages………………….**

**Uk 13**, wanaulizana habari tofauti tofauti kuhusu nyumbani, ndipo Akida kamwelezea kufeli kwa Tamari mitihani, Tim akamwambia eti" kila mwaka nyie mwapata mazo bora kuliko wazee wangu..

**Uk 14**, anaona friji mara yake ya kwanza ingawa alikuwa akisoma vitabuni. Pengine, David kwenda ghafla anapoonana na Tim mkahawani kwani alikuwa na deni lake la muda.

**Uk 15**, Tim anamfurahIa Akida na kumwambia **eti atasoma na kuwaprofesa kwa maporofesa..**

Uk 16, Akida alipoona wanawake waliokuwa nusu uchi…………. Wakati wanapokwenda kwa Tim shauri moyo………….

**SURA YA TATU**

Tim alikuwa anafanya kazi ya ukarani kwenye kiwanda cha kusindika mafuta baada ya kufeli mitihani…. Uk18

Uk 18, Akida kutumia Taulo na kuoga maji ya bafu la manyunyu mara yake ya kwanza na akashangaa sana Uk 20, Akida anamuuliza nani pichani? Naye Tim akamwambia eti ni dadake wa kirohoni….pamela kutoka sangura.

Uk 20-23, Akida kumtembeza jijini kokote baada ya kumwomba ruhusa mjombake kazini……….

Uk 23, kumtembelea mjombake Tim na kumkuta msichana mdogo akisoma kitabu "**war and peace**" na Akida akama viatu vyake ambavyo vilikuwa na mnuko kama mayai yaliyooza waliokuwa wakitazama filamu walidai…………………… Uk 24.

Uk 28, mjombake Tim kuja na kawasalimu—Tim kumjulisha kwa mjombake na akasema Akida kwa ni mkanju mjombake akakasizika akasema "**Hakuna mjinga kama mkanju…… mimi sifihi kitu …. Babako ana wanawake wangapi? Akamuuliza naye akasema Akida mmoja ……… uk 26 akaendelea hana number two?" mkani wa aina gani? Wakanju wanapenda mazishi………."**

Uk 27, Tim na Akida kufanya mradi na mipango ya kutembelea ofisi ya Bwana Gembo, Hatubagui publishers…..

Uk 28, 29, 30 , Habari ikatolewa kuwa vita vya kikabila vimeendelea wilayani korosho hasa eneo la Baraki na watu kunawa, Tim akakanusha habari hiyo…….. na kulikuwa na propanganda kwani sauti ya kiwachema husema hakuna vita na BBC, husema vita vimepanda moto….. uk 29.

**Sura ya nne**

Tim kwenda kazini na Akida kwenda jijini kutafuta gazeti lakini kwa bahati mbaya hakupata kitu, polisi ikawafukuza wauzaji wa magazeti………. Uk 31, na **Akida kupotelea njiani kuelekea shauri moyo- wa Tim. Vilevile, Akida kuona vigoli vikichizea mtaroni na kuambiwa eti, usivione vidogo hivyo**….. maze **usiku vina kwenda na wenye pajero na mabenz…. Uk 33**

**Uk 33,** Akida kumpumzika kidogo baada ya kuchoka kwa matembezi na viatu vyake alivyomwazima shemejiye – Tim kuibiwa ndipo akasema " **chaka la simbahalilali nguvuwe".** Baadaye akakutana na binti mrembo aliyemsaidia kwa kumwonyesha barasbara kuelekea shauri moyo ,,,,,… **Uk 34.**

**Sura ya tano**

Tim na Akida kukutana nyumbani na kujitia kwa utani "**Nilidhani mambo ni yamkono kumbe ni ya upembo**……. Uk 35 Akida akifanya mzaha kwa Tim.

Uk 35-36, pam kipenziche Tim kamtembelea na kukumbatana kwa mapenzi sana **"uchumba piani wakati wakufumbia macho makosa ya mchumba**. Wakati wa kujikiri mtu ni maasumu. Hukumbuki Kasisi John alivyotahadharisha kwenye mahubiriye mara nyingi ?

Kuwa wakristo wanaochumbiana waweza kupoteza udhibiti wa utashi wao- **wakijikuta wamefanya dhambi kama vile Daudi alivyofanya na mkewe uriah …….uk 36**

**Uk 38**, Akida kuwaimbia ubeti mmoja wapo wa wimbo wababake; na wote wakzana mapenzine.

Uk 40, kwenda kwa bwana Gembo, Akida na wenzake kuuliza malipo ya bima ya mamake aliyekufa ajalini lakini sekretari hakuwapatia ufadhili wowote labda akaendelea na kazi yake ndipo Akida akakumbuka shairi la babake alilomtungia kuhusu hasira kwani alikuwa karibu afanye jambo la ajabu………. Uk42

Watu wote wakasema, tumechoka mpaka tuonane na bwana Gembo atulipe pesa zetu…….. mzee matuko.

**Sura ya ya sita**

Akida na Pam kuenda kwa afisi ya waziri wa elimu kuzawadiwa. Akida alikuwa watatu nchini, **Donald Kitenge** ndiye aliyekuwa wa pili na **msichana Regina ndiye** aliyebwaga wote mtihani waTaifa…….Uk 50.

Uk 51, vilevile, wanaongozana hadi ofisi ya hatubagui publishers na kukuta mswada wa babake ulikuwa umetumwa kwake kwa njia ya posta….Uk 52.

Uk 57 Akida kupoteza zawadi yake garini

**Sura ya saba**

Asubuhi na mapema, Akida yuko nyumbani kwa Tim, akawaza nakuwazua matendo. Yaliyofanyika kumkamata mikononi waziri wa elimu yeye mwenyewe na kupoteza zawadi yake garini…….uk 58

Anasoma kitabu cha babake, kero za mkiwa, mawazo juu ya kijiji cha Baraki na kiwachema yakazidi , kwani Tom biniye **mzee mangala** akawelezea habari kuhusu kwao………. Tom akaoa mzungu…… uk 59.

Wote waamezama kwa mawazo tele baada ya kusikia habar ikuhusu vita vya kikabila na kudai kuwa wadadisi wa mambo wanasema. Ingawa makabila hayo mawili yamekuwa na chuki **baina yao, huenda vita hivyo vimechochewa na watu wenye usawishi mkubwa wa siasa…… uk 61**.

Uk 62, kifo cha matuko aliyejitupa kutoka ghorofa (22) ya Tembo House baada ya wakili wake Bwana Tony Gembo kukataa kuonana naye juu ya malipo ya bima yake.

Sasa, Akida yajiuliza iwapo ataweza kuwa na bahati ya kwenda kwa shule ya taifa, …… Uk 65, ***nipande ghorofa nijitupe kama mzee Yusufu Matuko?................*** Akida akaanza kujiuliza.

**Sura ya nane**

Pam anamkaribisha Akida na kumjulisha kuwa Tamari yu mgonjwa ……………. Uk 67, kuleta habari **kuwa kwao Baraki wilayani korosho vita vimepamba moto.**

**Habari ya kifo cha mzee sululu** kuwa maiti yake imelazwa kwa mochware na Akida kwenda kwa hospitali nakukagua maiti hiyo nakusema kuwa si babake…… Uk 70-71

**Sura ya tisa**

Wakaaenda hospitali ya Rufaa ya Tandika iliyojengwa wakati ule giza la ukoloni na wakakuta wagonjwa wengi kutoka korosho wamelezwa papo hapo kwamfano mzee **uledi ambaye bintiye Regina alisoma naye Akida darasa moja huko Baraki, wanafunzi wangemwiita Regina "mtawa"** kwa jinsi alivyojitenga kabisa na mambo ya kimapenzi……uk 74. Na mzee uledi akielezea namna alivyomsawisha mzee sululu ili waepuke vitisho na vita vya wakorosho lakini mzee sululu hakuweza…..uk 78.

**Sura ya kumi.**

**Tim na Akida kumtembelea Tom mtotowe mangala mwenye, bibiye mzungu….. Jenelle**, wakati wanapotoka kwa Rufaa ya hospitali.

**Vilevile , kifo cha kighafla cha mzee mangala**……. Uk 85 mwili wa mzee mangala ulikuwa katika hospitali ya nduchi ……..Uk 86 -. Uk 90, wakidai kuwa watupilie mbali majina kama sululu au mangala kwani yatambulisha sana kikabila.

Uk 91, Tom kufanya mradi wakumzika babake- mzee mangala na polisi ili waweze kuwasindikiza mpaka Baraki ili wamzike mzee mangala kwa heshima.

**Sura ya kumi na moja**

Tom, Akida kwenda kwa mazishi ya Mzee mangala na watu wengine wakisaidiwa na polisi.

**Vilevile:** kuona namna watu walivyoUawa huko Baraki. Akida akiona mabadiliko ya kwao.

Uk 99, Tom kusema **"Baba kama ungalikuwa umesoma" ungalikuwa umewahi kumsikia Antonio. Antonio ndiye aliyesema juu ya mwili wa Juliasi kaizairi " nimekuja kumzika sio kumsifu kaizairi…."**

Tom, kumwahidi Akida kuwa angemfanyia mpango wakwendaCanadaa iliasomee huko kwani ni mtu mwenye vipawa…… Uk 101, na kumwahidi kuwa akitaka kumwoa mzungu ni hiari yake. Naye akasema " **nioe muzungu, nizae wazungu hata wakiitwa chotara, eeh!! Kuoa mzungu! Nitakuwa wa kupigiwamfano kamaTom.**

Vile vile wanapotoka mazishini kunazuka ubishi wa ukabila garini wakimtusi dereva kuwa yeye ni mchungwachungwa…..

**Sura ya kumi na mbili**

Akida kumkomboa Tom wakati anapolala chini ya mwembe na kumtia kwa Toroli wakati wakorosho wanaotaka kuwaua na kulikuwemo mzee Zablon ambaye **ndiye Rafiki wa kufa kuzikana – Tim….. Uk 107 kwani Tom alikuwa amepigwa mshale.**

Uk 108, mwenye gari kumsaidia Akida na kumchukuwa kwa korosho hospitalini na wenye gari hao ni wafanyikazi wa shirika la **"Action men"** linaloshughulikia kwa kutoa msaada kama; chakula kwa wakimbizi……… Uk 108. Na katika mwendo huo **ndipo wanapoona vipande vya watu vikitafunwa na mbwa kando kando ya barabarani**……………….

**Sura ya kumi na tatu**

Akida kwenda mtaa wa Falkland, maarufu kwa jina la kambi mchafu kwa simon mwenye duka liitwalo **Mla chake** ili aweze kumwelekeza kwa Tim aliye kuwa akiishi huko baada ya kufukuzwa kazini na mjombake kwa kuwa na uhusiano mkubwa na Akida- mkanju..

Akida anampa habari Tim kuhusu kupigwa mshale na kulazwa hospitali ya korosho.

Sasa Akida akitafuta kazi ya aina yeyote ndiyo maana akisema "**mshoni hachaguinguo yakhe……**' Akida kupatanatena naTamari aliyekuwa anamchukia sana mwanzoni. Tamari akasema " nisamehe kwa ufedhuli wangu majuzi yale. Amina hebu tuseme uhamasa wangu kwako tangu tukiwa shuleni… Uk 17 Tamari naye vilevile anamwibia Akida et

***Nakupenda bila kiasi***

***Mpenzi ondoea wasiwasi***

***Hayafi mapenzi yetu sisi***

***Hayaji ijapo kwa risasi…. Uk 118***

**Sura ya kumi na nne**

Akida kuzoea mtaani Falkland kama mwenyeji na kuishi na Tim kama ndugu yake wa ukweli … **Tamari naye vile vile angekwenda kuwafulia nguo matajiri ile waweze kupata riziki ……. Uk 119.**

Akida kukumbuka mahuburi ya kasisi John, kuhusu yale maneno yake ya uhalisia na hata ya ukweli kuhusiana biblia kuhusu uesherati, Daudi na Bathsheba, mkwe uri……Uk 121

Akida akiendelea kupatana na Tim kwa hali ngumu sana kwani bidhaa kama sukari, maziwa namkate wakaviondoa kwa orodha yao ya mahitaji, hivyo vikawa vitu vya starehe isiyokuwa lazima …uk 127.

**Sura ya kumi na tano**

Tamari kumsawisha Akida ili waingie mapenzini…… na kukumbuka mahubiri ya Juma pili moja pale mhubiri John alipowahubiri kuwa Yusufu alikuwa nzi aliyenaswa kwenye utandabui alipoaniwa na mke wa potifa………… Uk 128, Daudi na mke wa ruiah…. Navile akakumbuka maneno ya Tim " mimi nakuamini wewe, ten asana najua huwezi kufanya lolote kunidhuru…… uk 129.

**Tamari kusema eti Akida ni mbakaji – Uk 130, bada ya kutaka kuingia naye Akida mapenzini na kukataa na kni mbwa tu" Akida** yataka kutoka kwa Tim lakini Tim anakataa akasema hawezi kumwaacha ……….Uk 131

Uk 132, ndipo Akida akamziba kibao mzee Tito Tembo akidhani ni mzee Zablon aliyekuwa akijisifu kuwa ameua watu wengi huko Baraki………..uk 133

**Sura ya kumi na sita**

Akida kutorekea sangura baada ya kumpiga kibao mzee Tito Tembo akidhani kuwa ni mzee Zablon. Na njiani anakuta wanafunzi wa chuo kikuu cha Tandika barabarani baada ya kufanya mgomo na **kuteketeza magari matatu….. uk 138.**

**Wanafunzi wanadai kuwa wahadhiri wa kume wanawaangusha wanafunzi wakiume kwa kuwa hawana chakuwapa uk 138**

**Sura ya kumi na saba**

Akida kufika kituo cha Biashara cha binge na kukuta watu wakipiga foleni kwa duka moja asubuhi na mapema na akataka kuvuka foleni na **wakamwambia eti** " **wewe wacha kuruka foleni, wadhari sisi ni viatu..uk 144.**

**Akida kwenda kwa uchochoro kwa haja ndogo ………uk** 144.

Uk 146, Akida kwenda kutafuta kazi kwa mzee muyaka nakusikia sauti ya lugha asiyo jua akiimba yaani mtotowe mzee muyaka – Johnstone Jerumani ambaye ni zumbukuku.

Uk 147, Bi.Tina kupinga suala la tohara ya wanawake akidai kuwa wengi wao wanaanga dumia kwa mzungu huo.

Uk 149, muyaka, mzee aliyepigana katika vita vya dunia, kali sana akampatia kazi ya kufunga wanyama. Na ndipo msichana yuyule aliyemkuta uchochoroni akijisaidia anaporudi nyumbani na kumkuta kwao ….. **Cynthia bintiye mzee** muyaka kufanya "**home work**"

**Sura ya kumi na nane**

Akida kujigeza jina ili wasimtambue akajibandika jina la "**Kipande madodo"** ili wasimtambue hasa kabila lake… **uk 152**. Jerumani kupenda sana kandanda..

Jerumani kumwelezea kilichotokea na kufungwa jela na serikali ya ujerumani ndiyo ilikuwa inamlipia ufadhili masomo yake lakini ikaondoa baadaye kwani alikuwa amepewa nafasi kwa kuwa **"best student"**

Mzee muyaka kugombana na mtotowe jerimani kwa kumwita kichaa.

**Sura ya kumi na tisa**

Habari kutolewa kwa jarida mojawapo la shirika moja la kutetea haki za kibinadamu yakionyesha athari ya vita vya kikabila wilayani korosho …. **Uk 160 –161.** Katika habari hiyo kulikuwa **John Kasisi aliyekuwa akishtakiwa kwa kufadhili mapigano.**

**Uk 163**, Bi. Tina kwenda kwa mkutano wa kundi la wanawake linalopinga **ukeketaji wa sehemu za siri za wasichana na wanawake …..uk 164**

Jonhson Jerumani kutoroka nyumbani baada ya kumpiga babake na Akida kumpa msaada ….. uk 167

Uk 168, mzee muyaka kuibiwa na bunduki yake na kwenda akilia, na polisi wenye landrova wakaja nyumbani kwake na kumhoji na baadaye wakmchukua na Bi. Tina naCynthia wakalia sana lakini baadaye mama anauza ngo'mbe na kwenda kuwahonga polisi nakurudi jioni na mmewe wakishikana mikono …. Uk168.

**Sura ya ishirini**

Kipande madodo –Akida kutaka kuingia mapenzini na Cynthia lakini akakumbuka maneno ya mzee muyaka ili ajitahadhari na bintiye cynthia- lakini baadaye **akajingiza mapenzi na Susana rafikiye wa karibu Cynthia --- uk 169. Ingawa Susana baadaye** akakataa kusoma na kuolewa na Joseph mwenye biaskeli..

Akida kumtorosha **Cynthia kisu cha ngariba mpaka mjini sangura kwa biaskeli ya joseph ….. kwani anahofu sana kuwa angeweza** kufariki kwa tohara kama vilivyo kwa watu wengi siku hizo..

Akida kusahau kila kitu na hasa kila mtu na vile Tim Rafikiye wa kufa kuzikana baada ya miaka miwili kutoka Tandika – Uk 173 vilevile**, Akida kusikia kifo cha waziri Johnstone mabende aliyenawa, wakati anapokikiliza kwa redio yam zeemuyaka……..Uk 173.**

**Sura ya ishirini namoja**

Bi.mkubwa yaani mamake muyaka akafa tena kwa mwanawe baada ya mwezi kupita baada ya kuwa na hitilafu kubwa kwa kutotahiriwa wajukuu wake.

Matayarisho ya kupokea wageni wanaoletaposa ya nanayakoyanafanywa juuchini nambuzi kunawa …. Uk 175

Barua ikaletwa kutoka kwa mzee muyaka na Bi.Tina kuichukua mpaka kwa mkewe Joseph - Susana ili amsomee lakini akashindwa …. Uk 178, ndipo Akida akawasomea.

***Kwa wazazi wangu,***

***Hayawi hayawi huwa, Tangu kufanya uchumba na mchumba wangu wangu sikuwahi kufikiria kuwa mtego ungeweza kujiri. Alikuwa wangu mandhia Matamanio na mapendezi yake yalikuwa sawa na yangu. Itakadi na faja zake zilikuwa zafanana na zangu. Nilipomtazama mbele niliona mustakabali mzuri katika ndoa isiyo na doa. Ila sasa mbele hakwendeki. Pamepita hitilafu kubwa kati yangu na mchumba wangu. Nakutumai mmeipokea barua hii mapema ilimuradi kuepuka kuingia gharama ya bure kwa maana hatutakuja nyumbani kwa shughuli ya posa kama tulivyo kuwa temepanga. Niobee mungu anipe moyo wa subira wakati huu wenye utata.***

***Binti yenu mpendwa***

***Nana***

Akida kutoka sangura kwelekea mjini Tandika baada ya miaka mitatu bila kuaga kwani wote wamepigwa biwi la simanzi kwa habari kutoka kwa nana binti yao.

**Sura ya ishirini na mbili**

Akida kurudi Tandika na kujipeleka kwa kituo cha polisi na kujiripoti kuwa aliua mzee zablon na kushindikwa kwa jela.

Vilevile akawakuta wafungwa mbali mbali na wenye mashtaka Fulani Fulani. Na hakupata bughadha kali na askari poli kurani wakampa ufadhili …. Uk 190

Akida kua chiliwa uhuru kwa kesi alizokuwa nazo kwani mzee zablon alijina mwenyewe na hata mzee Titi Tembo ai akamsamehe kwa kumziba kibao badala yam zee Zablon………

Tim kukutana naye baada ya kartini miaka mitatu ilikuwa imeishatoroka tokea wakati Akida alipokwenda sangara.

**Sura ya ushirini na tatu**

Tim kuandamana naAkida mpaka mtaa wa Falkland.

Tim vilevile kumwelezea kwa mapenzi yake na Pam yakapata kisogo,

Tim kumwelezea kifo chababake mzee Zablon kwa kusitia kitanzi miezi michache iliyopita. Pia vifo vya ndugu zake na mamake katika vita vya ukabila.

Tamari na Tim kumficha Akida wakati watoto wa mzee Tito Tembo wanapowa wavamia kwao na kumvalisha gauni ya wasichana na baadaye kumpeleka mpaka kwa mtaa **wa mama nasambu** kwa shangazi ya Pam.

**Sura ya ishirini nanne**

Akida kufika kwa mtaa wa mama Nasambu ili kujisalamisha, Tamari kutoka baada ya kumfikisha huko . mara kwa mara Tim, Tamari wengekuja na kumtembelea huko.

Akida kumwelezea Pam, kuwa alifanya kazi ya kwa mzee muyaka ambaye alipigana kwa vita vya dunia na habari chungu nzima iliyomfikia kwa miaka hiyo mitatu.

Akamwelezea kuhusu kuvunjika kwa mapenzi ya Nana na mchumbake.

**Isitoshe**, Akida akifanya kama daraja la kuwaunganisha tena Tim na Pam tena.

**Sura ya ishirini na Tano**

Shangazi yake kumfukuza Akida yaani hamtaki na baadaye anaomba mzee Toili ambaye ni mlinzi wa kwake shangazi-Pam ili ampeleke kwao aweze kujificha vilivyo.

Pam angempa pesa ya matumizi huko kwa mzee Toili na baada ye kabisha habari ikaja Tom kukumbkuka ahadi yake ya kumpeleka ulaya ili- kusoma kwa kuwa ameichukia nchi yake ya kiwachema.

**Vilevile, Akida anashangaa sana kuona Regina mtawa bintiye ya maheremu mzee uledi akisiuza kimasomaso … uk 220.**

Uk 221, Pam na Tim, wameshikana mikono na kumpungia naye vile vile Akida anawapungia anapopanda ndege mara yake ya kwanza na kusema **"Niache nendeuzunguni nisome nioe mzungu ikibidi…………Uk 221)**

**Uk 222, Akida analia, akisema mbona nalia? Naiacha nchi yangu ambapo mimi ni mwananchi kindakindaki. Nichukie kiwachema ? ……………. Akisema kiwachema kwa heri kwa sasa usilie nisubirinitarudi…………….**

Wahusika na utambulizi

Wahusika wakuu

1.**Akida sululu (Mkanju)**

Ni mvulana wa Mzee sululu na Joan sululu. Ni mkanju kwa kabila na rafikiye wa dhati waTim. Alikuwa wa tatu katika mtihani wa kitaifa na akazawadiwa na waziri Bwana Kato wa elimu.

**Sifa/tawasifu /tabia/hulka**

1.. Ni mwenye hasira alimjeruhi mzee Tito akidhanii ni mzee Zablon kwa madai kuwa alikuwa akijivunia kwa kuwa amewauwa wakanju wengi.

2. **Ni mvumilivu** – alivumilia wakati Tamari alimsingizia kuwa ni mbakaji.

3**. Ni mwongo**: (a) Anamdanganya mzee uledi ya kuwa Tim ni msangura.

**(b) Anamdanganya B.Tina ya kuwa yeye ni mchungwachungwa.**

4. **Ni msiri**: Hakumwambia Tamari ya kuwa babake ndiye aliyekuwa akiwaua wakanju huko wilayani korosho.

5. **Ni msomi/mwerevu**: Ni yeye aliyekuwa wa tatu kitaifa mitihanini kwa shule ya msingi.

6. **Ni mwenye bidii:** Akida alifanya vizuri katika mitihani ya mwisho wa shule ya msingi na kizawadiwa na waziri wa elimu.

7. **Ni mwenye utu**: Akida anapomsaidia Tom baada ya kupigwa mshale na kulala chini ya mwembe na kumpeleka hospitalini korosho.

(b) Akida anamwokoa mzee muyaka anapoumwa na nyoka kwa matibabu zahanati na kliniki za sangura zilikuwa mbali tena zilikuwa na uhaba wa madaktari na dawa.

8. **Ni mtulivu**: (a) Tamari anaposema kuwa Akida ni mbakaji alituliza hasira yake na kutoka nje.

(b) Anapoona ofisi ya stesheni ya sauti ya kiwachema anashikwa na hasira na kutaka kuvunja kioo cha ghorofa hiyo lakini anaacha na kuenda zake.

9. **Ni mcha mungu**: (a) Akida alikuwa akienda kanisani kila juma pili na Tamari na Tim.

(b) Akida anafuatia maneno ya kasisi John anavyowahotubia kanisani kama kuhusu umalaya.

10**. Ni mwimbaji**: Akida anawaiimbia Pam na Tim wanapomsihi awaimbie.

11**. Ni msamehevu**: Akida anamsamehe mzee Zablon kwa kumuua Mzee sululu ambaye ni babake.

12. **Ni mzalendo:** Anasema ya kwamba akienda ulaya atasoma atatue shida za ukabila huko kiwachema.

13. **Mwenye mapenzi:** Aliamua kumpeleka Tom hospitalini isapokuwa amejeruhiwa namshale na akabaki hapo bila. Kusita mpaka wakati alipompeleka hospitalini.

14. **Ni mkatili:** Akida alimpiga mzee mmoja aliyefanana na mzee Zablon mapisi ambaye alikuwa akidaiwa kwa kuua wakanju.

15. **Ni mwenye wivu:** (a) Alipoona vile Tim ameendelea akamwonea wivu.

(b) Alionyesha pia wivu wakati anapomwona.

**16. mpatanishi**: Anajaribu kupatanisha Pam na Tim wanapokosana.

**TIM MAPISI (MKOROSHO)**

mtoto wa mzee Zablon mapishi, ni mkorosho na ni ndugu yake Tamari na hata mpenzi wa Pam.

1.. Ni mchezaji bora wa kandanda. Alikuwa anacheza sana mpira huko shuleni.

2. **ni mwenye mapenzi**

**-Anapendanana Pam ambaye ni mpenziwe.**

**-Alimpenda Akida sana na kumsaidia wakati wa shida.**

**-Anampenda dadake Tamari aliporudishwa shuleni kusoma.**

3. **Ni mwenye utu:** (a) Tim alimsaidia Akida na viatu alipoona kuwa ana miguu mitupu?..

(b) Alionyesha utu anapomlipa mchungaji wa mortuary nduchi ili waweze kutafuta maiti ya babake Akida.

4. **Ni mtilivu** (a) Hata baada ya kupigwa kalamu kazini aliendelea kuwa rafiki na Akida.

(b) Anamtuliza Akida baada ya mjombake sasmson Tangu kumtukana.

5. **Ni mcheshi** . Anacheka anapokutana na Akida akirudi nyumbani miguu yake mitupu bila viatu.

6. **Ni mwenye bidii**. Anaonyesha bidii yake wakati hana kitu ya kujikimu maisha na anaamua kuuza viatu vyake ili kujikimu maisha.

Ananunua vitu vipya baada ya kupita kazi ndogo ndogo.

7. **Ni mlinzi** : anamlinda Akida shuleni ili wanafunzi tundu wasimchokoze. Vilevile, anamlinda Akida wakati watoto wa Tembo wanapokuwa wakimsaka.

8. **Ni mwenye matumaini:** Hata baada ya kufutwa kazini anaendelea kujikimu maisha.

9. **Ni mwenye hasira**: ananyesha hasira yake baada ya shetesheni ya sauti ya kiwachema kueneza habari yenye uwongo.

10. **Ni mvumilivu**: anavumilia maishani mwake hata kama haendi anavyohitaji.

11. **Ni mwenye wivu:** (a) wivu wake unabainishwa anapoona Pam anamkumbatia Akida baada ya kupewa zawadi na waziri wa elimu Bwana kato.

(b**) Vilevile Akida anapofika** mjini Tandika mara yake ya kwanza na Tim kumwelezea kuwa shamba lao hutoa mazao mengi kuliko yao kila msimu na hata ng"ombe wao hutoa maziwa mengi kuliko yao.

12**. Ni mkarimu**: Anamsaidia Akida na viatu bada ya kuona kuwa viatu alivyo navyo vimeharibika. Anampeleka Akida hotelini aweze kula chakula.

13. **Ni mwazi**: anamwambia mjombake Samson Tangu kuwa Akida ni mkanju bila kumdanganya.

14. **ni mjasiri**: anampeleka Akida kwa mjombake Samson Tangu na kumwambia eti ni mkanju bado anaendelea kuishi naye hata akijua atachukiwa.

15. **Ni mwaminifu**: anamwamini Akida kwa kila kitu asemacho.

**Tom mangala**: ni mtoto wa mzee mangala ambaye ni bwanake **Jenelle.** Akasoma hadi akafika ulaya na kisha akafanya kazi na kampuni ya Anken

1.. **Ni msomi :** Inaonyeshwa wakati Tom anasemekana alisoma ulaya na kisha kufanya na kampuni ya Anken.

2. **Ni mwenye mapenzi: Yaani** anapendana na Jenelle na hatamzungu na kumwoa akida na Tom wana mapenzi ndiyo maana Akida anafanikiwa kwenda ulaya kusomea huku.

3. **Ni mvumilivu**: Hata baada ya kuambiwa eti babake ameuawa vitani korosho yeye hakulia bali alivumilia

4. **Ni mkarimu:** Anakubali kusafiri na Akida na Tim kwa kutafuta baba zao.

5. **Ni jasiri:** Anaenda kumzika babake huko katika eneo la vita bila uoga wowote.

**6. Ni mtu mwenye bidi**

**7. ni mwenye utu.**

**8. Ni mwasi (Rebellious)**

**9. Ni mwaminifu.**

**10. Ni mnyamavu.**

**11. Mzalendo**

**MZEE MUYAKA**: Babake Johnstone na Cynthia na mkewe ni Bi.Tina . Aliwahi kushiriki katika vita vya dunia vya pili na hutoka sangura.

1.. **Ni mjeuri**: Akida anapokuwa akitafuta kazi hamjibu wakati anapo msalimu . Hakujali kuhusu maisha ya mwanawe Johnstone Jerumani.

2**. Ni mwoga**: Anaposikia kitu kimeanguka anajificha chini ya meza…………

3. **Ni shujaa**: Kwa kuwa alipigana kwa vita vya dunia.

4**. Ni mnyonge wa afya** .

5. **Ni mnyamavu:** Anamnyamavu wakati Akida anakuja kutafuta kazi.

6. **Anaongea vibaya kuhusu mtotowe** Johnstone Jerumani kwa kkuwa ni mwkenda wazimu.

**PAMELA** ni mpenzi wa Tim na alikuwa akiishi na shangazi yake eneo la mama Nasambu

1.. **Ni mpatanishi** Anajaribu kupatanisha Akida na Tamari baada ya Tamari kusema kuwa mzee sululu amena babake.

2. **Ni mcheshi**

3**. Ni mwenye utu:** Akida alipoletwa kwao na Tamari yeye alikubali ku mchunga.. Alipowaona watu wenye silaha nje ya nyumba yao anakuja na kumwambia mpenziwe Tim.

4. **Ni msaliti /mhafidiana**: Anasaliti mapenzi kati yake na Tim.

**5. Ni mcha mungu**: Anaenda kanisani kwa ajili ya ibada kilaJuma pili.

6. Ni mwenye utu: Anamlurumia Akida anapomwona kuwa ana wasiwasi na Tim , anapendana na Tamari na hata Akida .

8. Ni king'ang'anzini.

**Mzee sululu**: Babake Akida na ni mume wa Joan sululu. Alizaa watoto wengine lakini wote walifariki kabla ya Akida kuzaliwa.

1.. **Nimwenye utu**: Anamponya Tim anapoumwa na nyoka.

2. Ni **mwimbaji hodari**: Kwani ni mtunzi wa nyimbo na hataanataka kukchapisha mswaada wake .

3. Ni mjasiri.

4. Ni mwenye muamananawatu: Anamfundisha Akida jinsi ya kumtibu mtu anapokuwa mgonjwa.

5. Ni mwenye bidii

6. Ni mpweke

7. ni mhariri

8. Ni mpenda amani

9. Ni msomi: kwani anajulikanasana kwakuandika vitabu vya ushairi.

**JOAN SULULU:** mke wa mzee sululu mama yake Akida. Aliangaa dunia miaka lo, iliopita baada ya basi la abiria kupata ajali na lori Tungule kilimani . Alikuwa anauza samaki, matunda nk kiduka cha Baraki huko Korosho

**MZEEULEDI** : Ni mkanju aliyenusurika kifo na kukimbilia Tandika baada ya vita kuzuka , baba yake Regina

1**.. Ni mlevi**: Wakati Akida na Tim walipokuwa wanamuliza kamayeye ni mzee Uledi mwanamume mmoja akamwambia kuwa alikuwa ametindi.

2. Ni mwenye hasira

3. Ni mkatili

4. Ni mwenye bidii

5. **Anapenda ukabila**: Ilibainika wazi wakati alipouliza Tim ni kabila gai na Akida akamdanganya na kuanza kupayukapayuka.

**6. Ni mcheza marimba na gitaa**, yaani anawaambia Akida natim eti wakati waliporamiwa na wakorosho alikuwa akipiga gitaa yake.

7. Ni mwenye taasubu ya kiume

8. Ni omba omba

**Regina eledi:** mtoto wa mzee uledi na alikuwa akisoma darasa moja na Akida.

1.. Ni msomi

2. Alikuwa mtawa – Hakupenda mambo ya mapenzi.

3. Kahaba

4. Mhafidina/msaliti

**Tamari:** Mtoto wa mzee Zablon, na mdogo wake Tim, alimusurika kifo kwenye vita baina ya wakerosho na wakanju.

1.. Ni mwongo: Anadanganya ndugu yake Tim kuwa Akida alikuwa anataka kumbaka . anadanganya kwamba Babake Akida ameua Babake-mzee Zablon.

2. Ni ujinga.

3. Ni mwenye bidii

4. Ni usomi

5. Ni mtafutaji- Anafulia watu nguo kwenye maeneo ya uatajiri ili apate riziki.

**MLINZI TOILI**: Mlinzi kwa shangaziye Pamela – mtaa wa mama Nasambu.

**ROSE NA TIM**: Ni wanachuo kikuu cha kiwachema ambao walifukuzwa kutokana na migogoro ya cheshi na walipendana.

**MZEE KIJOKA**: mzee anayeelewa kabla ya kwenda kwa mzee muyaka. Ni mkali.

**JOSEPH:** aliyemoa susan rafikiye Cynthia

**SAMSON TUNGU** : mjombake Tim. Ni mkabila, mkarimu, ni mwazi nk.

**MAUDHUI**

**Ndoa ,** Ni wakati watu wawili wanaishi Pamoja wakishaoana na mapenzi. Ni mahusiano ya kikaribu kati ya watu wawili .

**Mapenzi:** Mapenzi kati ya Akida naTim nak walikuwa watu wa kabilatofauti (mapaenzi ya kufa kuzikana)

2. Mapenzi kati ya Akida na Tom (Kufa kuzikana )

3. Mapenzi kati ya Pam na Tim (mapenzi ya kawaida )

4. Mapenzi kati ya Tim na babake Mzee Zablon mapishi.

5. Mapenzi kati ya Pam naTamari.

6. Mapenzi katiya susan na kipande madodo.

7. Mapenzi kati ya Johnstonenakipande madodo.

8. Mapenzi kati ya nananamchumbake.

9. Mapenzi kati ya Bi. Tina na biniye Jerumani

**Ndoa** (1) Ndoa kati ya Joan Sululu na mzee Sululu

2. Ndoa kati yam zee Zablon na mkewe.

3. Ndoa kati Ya Joseph na Susan.

4. Ndoa kati ya Bi. Tina na mzee muyaka

5. Ndoa kati ya Jenelle na Tom.

**Ukabila:** Ni mapendeleo ya mtu Fulani kwa kabila lake. Kabila zinazopatikana kwenye kitabuni wakorosho nawakanju wachungwachungwa, wasangura nk.

1). Askari alipokuwa mwandamani wa Akida aliposema " **nakwambia hakuna watu zumbukuku kama wakanju.**

2) **Mjombake Tim- Samson tungu anapomtu si Akida akisema waknju wapenda mazishi sijui mazishi ya shangazi mjomba ….. nk hata wataanza kwanda mazishi ya mbwa.**

3) Vilevile, Tamari akionyesha ukabila anaposema Babake Akida ndiye aliyeua babake.

**Mazingira**: Akida anapoenda Tandika mara yake ya kwanza, anapoenda Sangura kwa mzee muyaka.

**Ugonjwa**: mwalimu Alex na Jerumani.

**Utamaduni**: kupashwa tohara.

**Umri** wa kuoa

**Malenzi**: Mwanamke alikuwa na jukumu la kuwalea wanawe.

**Elimu** : wanawake hawakupewa nafasi ya kupata elimu.

**Swali**

**"Migogoro ni chanzo cha maangamizi katika Jamii" Jadili**

**Kuna mifano mwafaka katika Riwaya.**

- Kati ya wakanju na wakorosho
- Kati ya Akida na Tamari

- Kati yam zee Muyaka na Bi.Tina mkewe.
- Kati ya Akida na Tito Tembo.
- Kati ya Tim namjombake – Samson Tungu
- Kati ya Pam na mpenziwe – Tim
- Kati ya mzee Matuko na sekretari
- Kati ya mzee Sululu na mzee Zablon
- Kati ya mwalimu Alex na mheshimiwa Johnstone Mabende.
- Kati ya serikali na vyombo vya habari.

**Swali**
**"Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu" Jadili methali hii ukirejelea Riwaya hii**;

Maana ya methali, Akida alipata nafasi ya kwenda ulaya kwasababu ya Rafikiye tim aliyemfanta ajuane na Tom-

- Regina na babake mzee uledi.
- Mzee Zablon mapisi na tim.
- Mzee muyaka na Johnstone Jerumani
- Mzee Sululu na Akida.
- Mzee mangalana Tom.
- Tom nanchi yake kiwachema.
- Mzee Sululu na mkewe Joan Sululu
- Kipande madodo na mzee muyaka.

**Swali:"Hakuna chuki katika Riwaya ya kufa kuzikana ila ni mapaendeleo katikakabila " Jadili.**

**Chuki** ni kuwa na hisia mbaya kwa mtu.

- Wakorosho na wakanju.
- Mbunge Jonstone mabende na wakanju.
- Mwalimu Alex na wakorosho wenzake .
- Tamari na Akida
- Mzee matuko na watu waliokwenda kwa Bwana Gembo kudai bima ya malipo yao na sekretari.
- Tito Tembo na Akida .
- Mjomba Samson Tungu na Tim.
- Mjomba SamsonTungu na Akida.

**Swali: "Ni nini nafasi ya Elimu katika Riwaya ya kufa kuzikana**.

**Elimu ni maarifa yanayo patikana ndani nanje ya shule.**

Mwalimu Alex alitumia elimu yake kutoleta vita wilayani korosho.

- Tom
- Akida
- Tamari
- Jerumani
- Mzee Sululu na mzee Zablon mapisi
- Tim

**Swali: "umaskini"**

"Kukosa vitu vya maana muhimu maishani

- Akida alikuwa masikini karasababu anapomfika Tim nampa nguo….
- Tim aliposhi mtaa wa Falkland
- Tajiri na masikini waishi hahali tofauti tofauti.
- Watu wanaishi kwenye nyumba ya nyasi wilayani korosho.

**Mbinu za lugha**: Ni njia ambazo mwandishi ametumia lugha ili kuwasilisha ujumbe wake;

**a). Mbinu rejeshi (Kisengele nyuma /Dambini) mbinu ya kurejelea mambo yaliyopita.**

Akida anaporejelea kifo cha mamake katika ajali miaka 10 iliyopita kwa ajali. Vilimani Tungule.

Akida akiwa stesheni ya polisi alivyofista. Ki kuwa alimwua mzee Tito Tembo akidhani kuwa ni mzee Zablon.

Mjini Tandika Akida anakumbuka maisha shuleni na Tim. Anasema akisema kuwa Tim alikuwa Mchezaji bora wa soka na wasichana walikuwa wanampanda

Mzee matuko anurejelea jinsi ahivyokuwa kwenye ajali iliyotokea huko Tungule vilimani.

- Tim alivyoumwa na nyoka.
- Akida anarejelea kuhusu mwalimu Alex
- Barua yam zee Zablon inarejelea majuto kwake kwa kumuua mzee Sululu ambaye kwa hakuna nakosa lolote.
- Akida na Pam wanarejelea mambo yaliyokuwa huko sangura.
- Akida anarejelea mambo yalivyokuwa Baraki na maneno ya Johnstone Mabende.
- Akida anarejelea mahali mamake alipokuwa akiuza bidhaa zake kama; samaki wakati walipokuwa watoto.

**b) Taswira**, ujenzi wa picha akilini mwa msomaji.

- Akida alivyoleza vile mwalimu Alex akirukwa na kichwa.
- Akida alipokuwa akienda mjini Tandika anajengapicha kwa masomaji jinsi mamake alivyo kufa kwa ajali.
- Mbwa alivyokuwa akila kichwa cha mtu huko Baraki wakati wa vita.
- Akida alipomwiimbia Tima na Pam.
- Akida alivyozawadiwa nawaziri wa elimu Bwana Kato.
- Akida alipompiga mzee Tito Tembo akifikiria kuwa mzee Zablon

**Ch)Uzungumzaji nafsi**: ni mbinu ya lugha ambayo mhusika huonyeshwa kimoyomoyo tim kusahau zawadi yake kwenye gari alisema "huyu Tim kumbe **limbukeni hivi? Vipi anaachia zawadi yangu kupotea vivi hivi tu? Na zawadi yenye nilikuwa hata sijafungua.**

**Jiji hili silijui wala nyuma yake nitafanyeje? … Akida a**napofika Tandika.

Akida akiwa kwenye mkahawa naTim alisema **"Tahau ola ladha nzuri ajabu**" watu wamashambani yanatupita mambo mazuri hayo? Au ni upya wa mambo?"

Akida alipokuwa kwa mjombake Tim, alizungumzia nafsia akasema….. ama alitakakuonyesha mali na amuali zao?

**Sadfa**: Vitu viwili kutokea wakati mmoja bila kutorajiwa.

Tim kuenda mahakamani . Akida akisubiri kusomewa mashtaka.

Akida na tim wakienda kwa tom. Tom naye akapata habari ya msiba.

Akida anapoenda klabuni.

Tito tembo anapokuwa klabuni akinywa .

Akida kuzaliwa na kupata vitabu mzee Sululu.

Akida kwenda ofisini ya Bw. Tembo na mzee matuko kuwepo.

Akida kupanga kurudi nyumbani, habari ya mipango kutambaa.

Habari kusambaa, Tamari kufika kwa tim.

Tim na Akida kwenda hospitalini, mzee uledi akiwa anatibiwa.

Akida kujisalamisha polisi, Kasisi John akiwa Jela.

Akida na tom kurudi Baraki, vita vikiwa bado havijamalizika.

Vile vile Ken Walibora ametumia mbinu nyingine kama:

**Tashbihi**

**Kinayas**

**Barua**

**Dhihaka /tabaini nk, ili kuwasilisha ujumbe wake**

## UTENGANO.

### Utangulizi:

Utengano ni riwaya iliyoandikwa na Said A Mohamed, mwaka wa (1980),na inazungumzia juu ya utengano kati ya wahusika mbalimbali. Kwanza kabisa kuna utengano kati ya bwana maksuudi na bi Tamima, Kazija, Mussa, Farashuu, Mwanasururu, Inspekta Fadhili na jamii nzima. Pia kuna utengano kati ya maimuna na mazingira. Na pia, kuna utengano kati ya watu na maisha yao ambao ulisababishwa na vifo.

Riwaya hii ya utengano kwanzia mwanzo hadi mwisho wake, inazungumzia juu ya utengano na mabaya yake. Na ilitungwa kwa ploti ambayo si ya moja kwa moja. Namna maimuna anavyohama kutoka sehemu moja hadi nyingine, ni dalili tosha ya utengano wa maisha yake na mazingira hayo anayotengana nayo. Na mhusika mkuu katika hii riwaya ni Maimuna kwa kuwa riwaya nzima imejengwa juu ya maisha yake.

### Dhamiira kuu ya mwandishi:

Dhamira huwa ni wazo kuu au ujumbe mkuu wa mwandishi au mzungumzaji. Lakini sasa kwa mkutadha wa riwaya hii, dhamira itajitokeza kama wazo kuu au ujumbe mkuu wa mwandishi. Dhamira kuu ya mwandishi ni kutuonyesha mabaya yanayotokana na kutengana pamoja na uchuu. Yote ambayo yanapatikana humu riwayani ni zao la uchuu yake Bwana Maksudi pamoja na utengano aliouweka kati ya nafsi yake, familia yake na jamii nzima.

### Uchambuzi wa picha la jalada:

Jalada ni karatasi ngumu inyowekwa juu ya kitabu na kuandikwa anwani ya kitabu, jina la mwandishi na la mchapishaji. Picha ni sura ya kitu au mtu ailyochorwa kwenye karatasi au kadi. Kwa hivyo, picha la jalada ni ile sura ya kitu au mtu iliyochorwa kwenye karatasi au kadi. Kulingana na riwaya ya utengano kitabu kipya, kuna picha ya mwanamke ambaye anakimbia na nyuma yake kuna moto na mbele yake kuna maji. Maana kwamba anakokimbia na anakokwenda ni sawa. Yote ni matatizo. Kulingana na kitabu cha kwanza cha utengano, kuna sura ya mwanamke mrembo ambaye amepiga nyumba mgongo maana kwamba ya nyuma hajali.

### Ploti:

Riwaya hii ya utengano iliandikwa na Said A Mohamed mwaka wa (1980), na inahusu utengano aliouweka bwana maksuudi kati ya familia yake na jamii nzima, na kati yake na jamii. suala ambalo hapo mwisho linasababisha uharibifu wa kile kizuri alichofikiria kuwa alikuwa anafanyia familia yake na yeye mwenyewe. Pia tunaona utengano wa maisha na dunia kwa mfano utengano wa mwanasururu, kitoto chake bwana maksuudi na maksuudi mwenyewe pamoja na maisha yao.

Kwanza kabisa tunaona bwana maksuudi anawatunza wanafamilia yake kama watawa. Anawachungia ndani nyumbani bila wao kutoka. Ikiwa wanataka kitu kutoka nje lazima wamtume mtumishi au waondoke naye bwana maksuudi mwenyewe. Siku moja, anatoka kama ilivyokuwa kawaida yake na kumdanganya mkewe bi Tamima kuwa anaenda kuzuru kaburi ya shehe wake akafanye ibada, na moja kwa moja akaenda kwa kazija. Huko ndiko anakutana na mussa mwanawe na kurushiana makonde na pengine kuumana (UK 14).

Wakati maksuudi anapotoka nyumbani, bi Tamima ambaye ni mjamzito mambo yanamwendea vibaya yaani wakati wakujifungua ushafika. Lakini hatoki kulingana na sheria za nyumba wala haruhusiwi kuingiza mkunga mle ndani kumsaidia kujifungua. Mwanawe wa kike, Maimuna anachanganyikiwa kwa maumivu ya mamake. Maimuna pamoja na biti kocho wanaamua kutoka nje waende na kumletea bi Tamima mkunga amsaidie kujifungua. Wanaenda kwa Farashuu na kumchukua kwake maksudi ili amsaidie Bi Tamima kujifungua na anapofika hivi hivi, anamkuta Bi Tamima tayari tayari na punde si punde, anazaa kitoto kiume(UK 34). Lakini wakati maimuna anapotoka na biti kocho kuelekea kwake farashuu, kuna mengi wanayoyaona njiani na kumsukuma na kuinua utashi na kiu yake ya kutaka kujua mengi yaliyo nje ya jengo la babake au tuseme jera. Biti kocho anamwahidi kuwa atamsaidia kutoroka kwao na aende kujipatia uhuru. Wakati wa farashuu kurudi zake, maimuna atoroka naye kama walivyoshauriana na kulala kwake usiku huo.

Baada ya maksuudi kutengana na kazija kwa sababu ya mussa mwanaye, anaamua kurudi nyumbani kwake usiku huo. Leo ni tofauti na kawaida yake ya kumaliza wiki nzima katika ibada zake. Ni kama zimezongwazongwa. Kufika nyumbani maksuudi, amkuta bi tamima ashajifungua. Swali ni; nani kakusaidia kujifungua? Bi Tamima hana neno. Ameshindwa na la kusema. Maimuna hayupo nyumbani tena, sasa nani kasaidia shughuli ya uzaazi. Zake maksudi zishapanda na kuanza kumcharaza na mkanda wake. Biti kocho huingia na kusema ndiye amemsaidia.

Bi Tamima apewa taraka na kufukuzwa pamoja na biti kocho kwa kosa la kuvunja sharia za nyumba na kumpoteza mwana-mtu na kuwaachisha kitoto kile nyumbani. Tamima aenda kwao na biti kocho aelekea kwake farashuu. Mipango yake farashuu ni kama inaendelea vizuri na asubuhi anampeleka maimuna kwake mama jeni pumziko, na lengo la kumtenganisha na familia yake. Huko, maimuna ashirikiana na Dora shoga yake. Lakini baada ya wakati, afumaniwa kwa kusema kuwa ameiba mali zake mama jeni.

Wakati hayo yote yanamfikia maimuna, babake bwana maksuudi anaendelea na shughuli zake za kugombea kiti pamoja na Siwa na Zanga. Wanapofika uwanjani wakiomba watu kura na ushabiki, maksuudi pamoja na afriti mwenziye bwana Zanga wanafumaniwa na raia. Wanawekwa pinguni na kupelekwa jera na inspekta fadhiri(UK 82).

Maimuna huendelea na uhuru wake ambao sasa hajui ikiwa ni uhuru au, mpaka kwa biti sururu huko Bobea ambako anatambulishwa na rafiki/shoga yake Dora kwa barua. Huko anaishi na kuanza maisha mapya akifanya kazi ya kuuza pombe pamoja na biti sururu. Kwa sauti yake nyororo, anapewa kazi ya kuimba Rumbalola hoteli na kuwa maarufu wa nyimbo na nataki(UK 109).

Habari hizi zinamfika babake, bwana maksuudi na anapanga safari ya kumtafuta mwanaye. Maksuudi anafiika bobea na kumwona mwanawe akiimba jukwaani. Anaamua kumfika lakini maimuna anakimbia. Watazamaji wanamgeukia maksuudi na kumpa cha mtema kuni. Maksuudi analazwa hospitalini na huko anakutana na Mussa mwanawe ambaye walifumaniana kwa kazija. Anamwelezea yote yaliyomfikia. Wote kwa pamoja; Mussa, Maksuudi, Rashidi na dereva wanaanza safari kwenda kwa biti sururu kumtafuta maimuna. Wanapofika huko, wanamkuta akipigana na kijakazi kwa kumsemea vibaya na kujivuna pamoja na shoka mpenzi wake(UK 143). Maksuudi ajaribu kumkataza maimuna mapigano lakini maimuna amgeukia vibaya na kumkataa kwa hasira kubwa akisema kuwa yeye hamjui na hataki kumwona tena mbele zake.

Kutokana na hayo yote, maimuna anaamua kutoka hapo tena na kuelekea futoni ambako anakutana na kabi na kuamua kuoana. Kabi huyu ni mjukuu wake farashuu. Kabi anamtumia habari farashuu kuwa amepata mwanamke na angependa kufunga ndoa naye. Farashuu anawatembelea wajukuu zake na kukuta mkewe kabi ni maimuna aliyemtorosha kwao kwa nia zake mwenyewe za kuitenganisha familiya yake bwana Maksuudi. Farashuu huishia kwa kujuta akikumbuka yale yote aliyomtendea mwana-mtu. Mwishowe, awapatia shamba huko liwazoni na kabi pamoja na maimuna waanza maisha yao mapya. Na huko liwazoni, mamake maimuna bi Tamima pamoja na Mussa wanamtembelea na kumwelezea juu ya kifo cha babake bwana Maksuudi.

## WAHUSIKA NA SIFA ZAO

1. **Maksuudi:**
    - Ni mhusika mkuu kwa kuwa anaendeleza matukio mbali mbali kwanzia mwanzo wa riwaya hadi mwisho wake.
    - Ni mumewe bi Tamima kwa kuwa tunaona anamtunza kama mtawa katika kasri yake.
    - Ni baba yake maimuna, mussa na kitoto.
    - Ni Malaya kwa kuwa tunamwona anamwacha mkewe nyumani na kwenda kwa kazija kufanya mapenzi naye.
    - Ni kiongozi kwa kuwa tunaona anafanya kazi ya mkuu wa wilaya ambapo anajilimbika mali nyingi kutokana na uongozi wake mbaya.
    - Ni mdanganyifu kwani, anamdanganya mkewe kuwa amekwenda kwa kaburi ya shehe wake, na yeye anakwenda kwa kazija. Pia, udanganyifu wake unapatikana pale ambapo awadanganya raia na kuwannyakua mali zao kwa mfano, mwanasururu binti yake farashuu.
    - Ni kaka yake inspekta fadhili.
    - Ni mwenye uchuu au tuseme tamaa kwa kuwa anajipendezea kila kitu. Na anapenda kitu kidogo anapokuwa anafanya kazi zake.
    - Ni mwenye miiko na sharia zake. Kwa mfano sharia za nyumbani kwake za kutotoka nje kwa watawa wake au kumruhusu mtu yeyote kuingia mle ndani.
    - Ni mwenye hasira. Hasira zake zinapatikana pale anapomcharaza mkewe kwa kumpoteza mwanawe kipenzi maimuna.

2. **Maimuna**
    - Ni mhusika mkuu naye kwa kuwa anaonekana kwanzia mwanzo wa riwaya hadi mwisho wake. Ndiye anayeendeleza matukio mengi katika riwaya hii. Pia, riwaya nzima imetungwa kadri anavyo tengana na mazingira mbali mbali anayotangamana nayo.
    - Ni mwana wao maksuudi na bi Tamima. Pia ni dada yake mussa
    - Ni mwenye kiu. Kiu ya kujipatia uhuru ambao unasababisha kutoroka kwake nyumbani kwao na kuelekea mahali asikokujua.
    - Ni mwenye huruma. Anamhurumia mamake wakati anapokuwa mja mzito na tayari kujifungua. Pia, anamhurumia Kabi baada ya kumwelezea yake yote wakati anataka kumfunga ndoa.
    - Ni shoga yake Dora ambaye wanakutana pamoja kwa mama jeni na kusaidiana kwa hali na mali.

- Ni Malaya kwa kuwa baada yake kushindwa maisha ya mjini, anaamua kutafuta riziki na riziki yenyewe ni kujiuza. Hali ambayo ni nipa ni kupe. Anafanya umalaya na shoka huko mjini bobea kwa biti sururu.
- Ni mkewe Kabi ambaye ni mvuvi na wanakutania huko futoni na kuanza mapenzi na kufunga ndoa na kuishi liwazoni ambapo wanapewa na farashuu nyanya yake Kabi.
- Ni mwenye hasira. Hasira zake zinapatikana pale ambapo anamfokea babake anapokutana naye kwa biti sururu akipigana na kijakazi. Pia hasira zake za kuchukia mambo zinamfanya ahame kutoka sehemu moja kwelekea nyingine bila kujali atakalokutana nalo huko anakokwenda.

3. **Bi Tamima**
   - Mkewe bwana maksuudi wa ndoa. Lakini ndoa yao haikuwa na furaha, ni ndoa kwa jina ambayo haipendezi hata kamwe.
   - Mama yao mussa, maimuna na kitoto.
   - Mwenye mapenzi na uvumilivu. Ingawa anateswa na mmewe, anaendelea kumpenda na kuvumilia kila teso.
   - Ni mwenye huruma. Kwanza kabisa anahurumia nafsi yake pale anapocharazwa vibaya na kuamua yeye apewe talaka. Pia, anamhurumia mwanawe wa kike wa pekee wakati anapotoroka nyumbani na kwenda mahali asikokujua.
   - Ni rafiki yake biti kocho ingawa biti kocho anamtumikia.

4. **Mussa**
   - Ni mwana wao maksuudi na bi Tamima wa kiume ambaye ndiye mkuu.
   - Mussa ni daktari kwa kuwa anamtibu babake baada ya kulazwa hospitalini alipopigwa na watu kule hoteli Rambolola.
   - Mussa ni mpenda wanawake. Hili linadhihilika pale anapomwendea kazija mama wa kazi kufanya mapenzi na kukutania huko na babake na kupigana.
   - Ni mwenye hasira. Hasira zake zinapatikana pale anapokuwa mvunguni mwa kitanda na babake anapoendelea kuchezacheza na kazija, na mara moja tu anajibwaga mbele zao bila kujua kuwa mwanamume yule yule ni babake.
   - Ni mpiga mtindi. Hili hudhihilika pale anapokuwa kirabuni anapokutana na kazija mama wa kazi. Na pia, anapokwenda kwake kazija, anapewa vileo na kulewa Zaidi.
   - Ni mwenye huruma. Anamhurumia babake anapolazwa hositalini kwa kumpa damu yake. Pia, anamhurumia dadake maimuna baada ya kuambiwa kuwa babake anamtafuta nay eye anajiunga na kikosi cha kumtafuta.
   - Ni msomi kwa kuwa tunaona baada ya kuvamiwa na babake kwa kazija, anaamua kubadilisha tabia yake na kuendelea na masomo yake mpaka anapokuwa daktari wa kutibu.

5. **Farashuu**
   - Ni mkunga wa kuwasaidia wajawazito kujifungua. Anafanya ukunga kwa nyumba yake maksuudi na kumsaidia bi Tamima kujifungua kile kitoto kiume.
   - Ni mama yake mwanasururu na nyanya yake Kabi.
   - Ni mfanya kazi kwa kuwa nyumbani kwake anafanya kazi mbalimbali mnamo kupika mkate. Ni mwanamke aliyetofauti na wanawake wengine.

- Ni mpenda kulipiza kisasi. Analipiza kisasi kwa bwana maksuudi kwa sababu ya kumyanyasa mwanawe mwanasururu mpaka kufa. Anapanga njama ya kuitenganisha familia yake maksuudi huku akisaidiwa na shoga zake, na njama yake anafanikiwa.
- Ni shoga yake kazija na mama jeni ambao tunaona wanamsaidia kutekeleza mipango yake ya kuitenganisha familia ya mtu.
- Ni rafiki yake tena shoga yake biti kocho. Anamheshimu kadri kwamba anamtumikia kama pale biti kocho anapokuja kwake kumchukua uganga, hakukataa. Anakubali ingawa anajua ugumu wa kule anapokwenda.
- Ni mwenye huruma kwa kuwa anawahurumia wajukuu zake na kuwapa shamba huko liwazoni wakaanze maisha yao mapya. Pia, hapo mwishoni mwa riwaya, anamhurumia maksuudi baada ya kusikia habari za kifo chake na kujiangalia kuwa yeye ndiye amesababisha.
- Ni mjua mengi kuhusu dunia, hili linapatikana pale anapokipa kile kitoto kionje kwenye utamu na ukali wa dunia baada ya kuzaliwa.

6. **Biti kocho**
   - Mtumishi kwa nyumba ya bwana maksuudi kwa kuwa tunamwona akitumikia bi Tamima, maimuna na maksuudi mwenyewe.
   - Ni mpenda uhuru kwa kuwa anamsaidia maimuna kutoroka kwao na kwenda kujitafutia uhuru wake. Na pia, anamsaidia bi Tamima kwenda zake akajipatie uhuru na atokane na mozongwe ya nyumba yake maksuudi.
   - Ni mwenye huruma kwa kuwa anamhurumia bi Tamima wakati anapocharazwa na bwana wake kwa kutumia ukanda, na kujifanya mkali kwa kusema ndiye yeye amefanya ukunga na kumsaidia mama-mtu kujifungua.
   - Ni shoga yake farashuu kwa kuwa anamsaidia kufanikisha njama zake kwa nyumba yake bwana maksuudi.

7. **Mwanasururu**
   - Ni mwanawe farashuu na mama yake Kabi.
   - Ni mkewe bwana maksuudi hapo mwanzo.
   - Ni mtajiri kwa kuwa tunaona utajiri wake ndio ulisababisha kifo chake kiasi kwamba maksuudi kutokana na tamaa yake nyingi anamtesa baada ya kunyakua kila kitu chake.
8. **Kabi**
   - Ni mumewe maimuna kwa kuwa tunaona akikubaliana naye na kufunga ndoa na kuishi pamoja kwao huko liwazoni.
   - Ni mwanawe mwanasururu na mjukuu wake farashuu.
   - Ni kilema kwa kuwa tunaona anatembeza mguu mmoja.
   - Ni mvuvi huko futoni ambako anakutana na maimuna na kumpa samaki.
   - Ni mwenye mapenzi kwa kuwa anakubali kumwoa maimuna licha ya matatizo yote aliyoyapiitia.
   - Ni mwenye mila na desturi kwa kuwa baada ya kukubaliana na maimuna kuoana, anatuma ujumbe kwa nyanya yake kuja na kuzungumzia hilo suala.
9. **Kazija**
   - Ni shoga yake farashuu kwa kuwa anamsaidia kufanikisha njama yake.
   - Anawachukia viumbe wa kiume lakini afanye nini kwa kuwa dunia inamtukuza mwanamume. Na pia, anaichukia nafsi yake.
   - Ni mpenda mabadiliko. Anachangia sana katika kumwachisha na kumwangusha chini bwana maksuudi wakati wa kuomba kula huko kwenye uwanja.

- Ni Malaya. Kwa kuwa anafanya mapenzi na mussa pamoja na baba yake. Si hiyo tu, anafanya mapenzi na maksuudi akijua kuwa anamke nyumbani.
- Ni mwenye huruma. Anamhurumia mwanasururu na kuchangia katika kulipaza kisasi kwa mamake farashuu.

**10. Inspekta fadhili**

- Ni askari polisi. Kwa kuwa tunamwona akiwaweka maksuudi na zanga kwenye pingu wanapokuwa wanaomba kura huko uwanjani.
- Ni mtu ambaye hapendi rushwa kwa kuwa anakataa kushawishika na kaka yake anapokuwa anataka usaidizi wake.
- Ni kaka yake bwana maksuudi na mjomba wao maimuna na mussa.
- Ni mpenda mabadiliko. Kwa kuwa tunamwona anatoa mchango mkubwa kumwangusha kaka yake maksuudi anapokuwa anagombea kiti na wenziye akina Zanga na Siwa.

**11. Rashidi**

- Ni dereva yake bwana maksuudi kwa kuwa anamchukua mahali Fulani Fulani akiwa anaendeleza shughuli zake.
- Ni rafiki yake wa dhati bwana maksuudi kwa kuwa hata baada ya maksuudi kupelekwa jela na kutoka, anamsaidia sana kuwatafuta watoto wake. Hakuachana naye baada ya mabadiliko.

**12. Bi sada**

- Ni mtumishi kwake bwana maksuudi kwa kuwa tunamwona akishirikiana na biti kocho kuendeleza kazi za mle ndani nyumbani kwa maksuudi.
- Ni rafiki yake bi Tamima kwa kuwa hata naye anaonekana akimuhurumia anapokuwa mjamzito wakati wa kujifungua.
- Ni shoga yake biti kocho kwa kuwa wanasaidiana kuficha yanayowahusu kwa mfano pale maksuudi anapowauliza nani kamsaidia mama kujifungua, hakusema.

**13. Mama jeni**

- Ni shoga yake farashuu kwa kuwa anamsaidia kufanikisha njama yake.
- Ni mwendelezaji wa biashara ya uhayawani huko pumziko.

**14. James**

- Ni Malaya kwa kuwa analipa pesa kwa mama jeni na kumnunua maimuna lakini maimuna anakata na james kudai pesa zake tena.
- Ni mwenye hasira. Hasira zake zinapatikana pale ambapo maimuna anamkataa na james kukasirika na kudai pesa zake tena kiukali.
- Ni msomi kwa kuwa anazungumza kiingereza. Mfano *come on* (uk 56)
- Ni mtembezi kwa kuwa anamwambia maimuna kuwa amepambana na mabahari makubwa, ya cairo, ya London, ya hong kong na kadhalika. (UK 57)

**15. Dora**

- Ni Malaya kwa kuwa anafanya kazi ya kujiuza huko kwa mama jeni.
- Ni shoga yake maimuna.
- Ni mwenye huruma kwa kuwa anamhurumia maimuna anapokuwa anatoka kwa mama jeni akienda mahali asikojua, na kumtambulisha kwa biti sururu.

**16. Biti sururu**

- Ni mwenye biashara ya kuuza vileo huko bobea
- ni mwenye huruma kwa kuwa anakubari kumkaribisha maimuna na kumpa malazi pamoja na kazi.
- Ni rafiki yake Dora.

**17. Shoka**

- Ni Malaya kwa kuwa anamwacha mkewe nyumbani na kumwendea maimuna na kijakazi.
- Ni mfanya kazi.
- Ni mpiga mtindi.

**18. Zanga**

- Ni mgombea wa kiti yeye pamoja na maksuudi
- ni mdanganyifu kwa kuwa anawahidi watu mengi wakimchagua, kumbe anawadanganya.

**19. Siwa**

- Kipenzi cha watu.
- Mgombea kiti yeye pamoja na zanga na maksuudi.
- Ni msema machache.

**20. Mzee japu**

- Ni mwenye hasira na hasira zake zinaonekana pale maksuudi na zanga wanapoomba ushabiki wa raia. Anawasema mengi.

21. **Mzee bakar**i naye ni mmoja wapo wa raia na mwenye hasira kwa zanga.
22. **Mama miraji** naye pia ni raia na mwenye hasira kwa wagombea kiti ispokuwa Siwa pekee yake.
23. **Biti Shomari** ni mmojawapo wa raia wanaoombwa ushabiki.
24. **Bi Mpikawali** ni mfanya biashara ya upishi ambako kwake ndiko shoka anapatia chakula anapotoka kazini.
25. **Selume** ni mkewe shoka.
26. **Kijakazi** ni Malaya yake shoka ambaye anapigana na maimuna.
27. **Mzee Munda** ni mteja kwake biti sururu na pia ni mpiga mtindi.
28. **Mwana** mkuu ni shoga yake maimuna huko futoni.
29. **Ashuru** ni mwenye biashara ya duka huko futoni ambako maimuna anapata mkopo wa bidha bila malipo.
30. **Bakari** ni jirani yake kabi huko liwazoni.
31. **Mariamu** ni mkewe bakari.
32. **Kitoto** ni mwana wao maksuudi na Bi Tamima ambaye anakufa kwa kukosa malezi bora baada ya mamake kufukuzwa nyumbani.
33. watu wengine

**MAUDHUI YALIYOMO**:

Maudhui ni jumla ya mambo muhimu na mawazo ya msanii anayolenga kuwatolea wasomaji wa kazi yake au hadhira yake ili kuwaelimisha, kuwakosoa na kuwafahamisha. Na katika hii riwaya ya utengano, kuna maudhui mengi ambayo hubeba mafunzo mbalimbali. Mmaudhui hayo ni kama yafuatayo;

- ✓ Utengano
- ✓ Uongozi
- ✓ Umalaya
- ✓ Taraka
- ✓ Utumisi
- ✓ Ukunga
- ✓ Ulipizaji kisasi
- ✓ Vifo
- ✓ Utoro
- ✓ Uhuru

- ✓ Udanganyifu/ uafriti
- ✓ Unyanyasaji
- ✓ Utawa
- ✓ Uvuvi
- ✓ Majuto
- ✓ Biashara

**Utengano**: ni tendo la kuachana au kukaa mbali na kitu kingine bila ya kushirikiana. Katika riwaya hii ya utengano, utengano unajitokeza kwa njia mbali mbali. Kwanza kuna utengano wa bwana Maksuudi na jamii nzima. Anajiona kuwa yeye ni mwenye uwezo kuliko wenzake na kujipendezea kila kitu. Pia, kuna utengano wa familiya yake maksuudi na jamii nzima uliosababishwa na maksuudi mwenyewe kwa kuwatunza wanafamilia yake kama watawa na kuwachungia ndani ya nyumba bila kutoka. (UK 19).

**Uongozi:** ni madaraka anyopewa mtu ya kusimama au kuongoza shughuli. Katika riwaya hii ya uengano, uongozi unajitokeza katika njia mbali mbali. Kwanza kuna uongozi ambao maafriti wawili yaani; bwana maksuudi na zanga, pamoja na siwa wanagobea. (UK 77). Pia, kuna uongozi wake bwana Maksuudi wa kuwa mkuu wa wilaya ambao anautumia kujiongezea mali kwa kuwanyanganya watu mali zao na kujilimbika yeye mwenyewe.

**Umalaya**: ni vitendo vya mtu yeyote vya kufanya uasherati. Na katika riwaya hii, kuna umalaya wa aina mbali mbali. Kwanza kabisa tunaona umalaya wa bwana Maksuudi. Mwenye familiya, mke yuko nyumbani lakini anamwendea kazija ili wakafanye mapenzi. (UK 11). Pia umalaya unapatikana pale ambapo Mussa naye anajiingiza kwenye mapenzi na kazija. Vile vile, kuna umalaya wake maimuna, mwana-mtu ambao aliingia bila yeye kujua kwa nataka za mjini na uhuru alioutamani. (UK 113). Kuna umalaya wa Dora shogaye maimuna, na kijakazi.

**Talaka:** ni maandishi au tamko analotoa mume wakati wakumwacha mke wake. Katika riwaya hii ya utengano kuna talaka inayopewa bi Tamima na mumewe bwana maksuudi kwa sababu ya kuvunja miiko ya familia na kumpoteza mwanawe kipenzi. (UK 53).

**Utumishi:** ni hali ya kuajiriwa au kufanya kazi kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa. Na katika riwaya hii ya utengano, kuna utumishi katika nyumba yake bwana maksuudi ambapo tunaona Biti Kocho na Bi Sada wanamtumikia mkubwa wao na wanafamilia nzima.

**Ukunga**: ni kazi ya mkunga kumsaidia mwanamke muda wa kuwa na mimba na wakati wa kuzaa. Katika riwaya hii, kuna ukunga pale ambapo tunaona Farashuu anamsaidia bi Tamima kujifungua na kikizaa kile kitoto ambacho ni cha uzazi wake wa tatu.(UK 34).

**Ulipizaji kisasi:** ni tendo la kumtendea vibaya aliyekutendea vibaya. Na katika riwaya hii ya utengano, ulipizaji kisasi unapatikana katika njama zake Farashuu za kuiangusha familia ya bwana maksuudi. Kwanza anampangia njama na shoga yake kazija iliakutane na bini yake kwake na watengane. Hilo linafanikiwa.(UK 14). Pia, anamtorosha mwana mtu kwao na hilo linafanikiwa. Pia anamfanya mke wa mtu apewe talaka na kufukuzwa nyumbani kwake. Yote haya yanasababishwa na matendo maovu maksuudi aliyomfanyia mwanawe Farashuu, mwanasururu yaliyosababisha kifo chake na toka huko, Farashuu kaamua kulipiza kisasi dhidi ya nyumba yake bwana maksuudi.

**Vifo/kifo:** ni hali ya kutokuwa na uhai au kukoma kupumua moja kwa moja ambapo kiumbe hai hupoteza maisha. Katika riwaya hii ya utengano, kuna vifo mbali mbali. Kuna kifo cha mtoto wake maksuudi ambaye anamwachisha mama yake. Kuna kifo cha mwanasururu ambaye ni mwanawe Farashuu. Pia kuna kifo cha maksuudi mwenyewe ambacho kinaambiwa kwa wote mwishoni mwa riwaya na kuwaliza akina maimuna na Farashuu.(UK 174 ,176)

**Utoro:** hii ni hali au tendo la kutoroka au kuondoka mahali mara kwa mara bila ruhusa. Riwayani, tunaona maimuna akitoroka kwao kwa sababu ya kiu yake ya kutaka kujionea maisha ya nje ya kasri ya babake. Kutoroka kwake kunasaidiwa na biti kocho pamoja na Farashuu ambao wanamhamisha mpaka mjini pumziko. (UK 41). Pia, maimuna anatoroka kwa mama jeni baada ya kusemewa kuwa ameiba mali zake mama huyo. Maimuna pia, anatoroka kwa biti sururu baada ya kupigana na kijakazi na kukutwa na babake bwana maksuudi. (UK 147).

**Uhuru**: ni hali ya kufanya jambo bila kuingiliwa na mtu au kuomba ruhusa lakini kwa kufuata sharia na kanuni zilizohusika. Au pengine, ni hali ya kuishi bila kutawaliwa na mtu. Kulingana na riwaya hii ya utengano, kuna uhuru ambao maimuna ana kiu kwake. Anataka ajitawale. Ajiamulie. Ajitunze. Lakini hajui aupateje?. Uhuru huu ndio unamsukuma kutoroka kwao kwa hamu ya kuuonja na kwenda asikokujua. Tunamwona anzama ndani ya uhuru huu lakini hapo mwiso anatambua kuwa alivyotamani havikuwa namna alivyotamania.

**Udanganyifu:** ni vitendo vya kughilibu watu au kufanya jambo ambalo mtu anajua ni la uongo. Katika riwaya hii ya utengano, maksuudi anamdanganya mkewe kuwa amekwenda kwa kaburi la shehe wake na kuwa atamaliza muda wa wiki nzima huko akifanya ibada zake, kumbe kwa shehe ni kwa kazija. Na zile ibada ni mapenzi ya kando kando au tuseme ya kupita njia. (UK 20).

**Unyanyasaji:** ni hali ya kukandamiza na kuonea wengine. Riwayani, bwana maksuudi anawanyanyasa wanafamilia yake kwa kuwatenga na jamii nzima. Pia, anawanyanyasa wanajamii kwa kuwanyakua mali zao na kula pesa za wenzake katika shughuli za kununua viwanja vya kujengea nyumba. Mfano mzuri hapa ni mkewe mzee japu (UK 78) na mwanasururu.

**Utawa:** ni hali ya kuishi maisha ya kiupekee kwa kukaa nyumbani mbali na raha za dunia. Riwayani, utawa unapatikana katika kasri yake bwana maksuudi ambapo bi Tamima na Maimuna wanatunzwa kama watawa. Hawatoki nje wala hakuruhusiwi mle ndani kuingia mtu bila maksuudi kujua au pengine yeye kukubali. (UK 19).

**Majuto**: ni hali ya kusikitisha inayotokana na kosa lililofanyika. Katika riwaya hii ya utengano, kuna majuto ya bwana maksuudi ambapo anajuta kwa kujitenga na familia yake kitu ambacho kinasababisha yeye kufungwa jela na kupoteza kazi yake.(UK 101). Pia. Kuna majuto yake farashuu kwa yote aliyomtendea mwana-mtu maimuna.(UK 176).

**Biashara:** ni hali/ shughuli ya kununua na kuuza bidhaa mbalimbali. Katika riwaya hii ya utengano, kuna shughuli mbali mbalimbali za uuzaji na ununuzi wa bidha. Kwanza kabisa, kuna biashara katika nyumba za siri huko pumziko ambako wasichana na wanawake hujiuzia ili kujipatia riziki. Pia, kuna biashara ya hoteli Rumbalola huko Bobea(UK 119). Kuna biashara za kuuza samaki kule Futoni kwake Kabi. Na biashara zinginezo.

Na maudhui mengine mengi ambayo ukisoma lazima utajionea na kuongezea kwa haya ambayo tumejaribu kukutolea. Cha muhimu ni kukumbuka kuwa haya maudhui ambayo huwa ni mambo makuu ya mwandishi, hubeba mafunzo kwa msomaji. Ni bora kuyachambua ipasavyo na kuona mkutadha wa matumizi ili uvuke na fahari ya najua ujumbe wa mwandishi.

**MBINU ZA UANDISHI:**

Mbinu ni namna ya kufanya jambo. Kwa mujibu wa uandishi, mbinu za uandishi ni namna mtunzi anavyo iunda na kuipanga kazi yake Fulani ya kifasihi. Na katika riwaya hii ya utengano, Said A Mohamed alitumia mbinu kadha kwa ufasaha wake ili kuwasilisha ujumbe wake na dhamira yake kwa wasomaji wa kazi yake hii. Mbinu alizozitumia ni sawa na:

- Mbinu ya masimulizi
- Methali
- Nyimbo
- Uchanganyaji ndimi
- Misemo
- Tashbihi
- Takriri
- Taharuki
- Majazi
- Utohozi
- Chuku
- Maswali ya balagha

**Mbinu ya masimulizi**: mbinu hii hujihusisha na maelezo ya jambo Fulani. Kwanzia mwanzo wa riwaya hadi mwisho wake, matukio mbalimbali husimuliwa. Mbinu hii humsaidia mwandishi kuendeleza kazi yake bila utata wowote. Matukio Fulani Fulani yanayoendelezwa na wahusika mbalimbali huelezwa hatua kwa hatua kulingana na kusudio lake mwandishi.

**Methali:** ni usemi unaoaminiwa kuwa na ukweli ambao huwa na maana iliyofumbwa isiyoeleweka kwa maneno yaliyotumika katika usemi huo. Kulingana na riwaya hii ya utengano, mwandishi alitumia methali nyingi zenye maana tofauti ili kuufikisha ujumbe na mafunzo yake kwa jamii lengwa. Mifano ya methali alizotumia mwandishi ni kama:

*Paka akiondoka panya hutawala (UK 42)*

*Siku anayokwenda uchi mtu, ndiyo siku anayokutana na mkwewe. (UK 46)*

*Penye unyonge mapambano hayeshi (UK 51)*

*Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki (UK 85)*

*Nia mbi huharibu, nia njema tabibu (UK 101)*

**Nyimbo**: ni maneno ya sauti zilizopangwa na zinazopigwa kama ngoma ambazo huwa ni muziki. Mwandishi wa riwaya hii ya utengano, ailitumia nyimbo mbali mbali na lengo la kufufikisha ujumbe Fulani kwa wasomaji wa kazi yake. Mara nyingi nyimbo hutumiwa kuweka msisitizo kwenye jambo Fulani linalowasilishwa kupitia kwake. Vile, hutumiwa kuwasilisha ujumbe teule wenye uzito kadri Fulani. Said A Mohamed, alitumia nyimbo kama zile za maimuna (UK 117)

**Uchanganyaji ndimi**: hii ni mbinu ya kutumia lugha Zaidi ya moja katika kazi Fulani ya kifasihi. Mara nyingi mbinu hii hutumiwa ili kuipamba kazi Fulani na kuifanya ipendeze Zaidi kwa wasomaji wake. Pia, humsaidia mwandishi kuhusisha baadhi ya maneno ambayo huenda akashindwa kuyapatia tafsiri iliyo sawa. Na katika riwaya hii, mwandishi alitumia maneno yasiyo ya Kiswahili kama vile*, Give……give me(uk 6), come on darling(uk 7), counter(uk 119)* na maneno mengine mengi.

**Misemo**: ni mafungu ya maneno yenye maana maalum ambayo hutoa mafundisho kwa jamii. Katika riwaya hii ya utengano, mwandishi aalitumia misemo kama vile: *cha mtema kuni* (UK 142).

**Tashbihi**: ni mbinu ya kufananisha vitu viwili au Zaidi. Mwandishi wa riwaya hii, alitumia mbinu hii ya kufananisha vitu viwili au Zaidi kwa kutumia neno 'kama'. Kwa mfano; kama mbwa mwitu mwenye hasira(UK 49), kama samba (UK 57) na mifano mengineyo. Tashbihi hutumiwa na wandishi mbalimbali na lengo la kuvunja tabia mbaya za watu mbali mbali katika jamii. Pengine, hutumiwa kuwasilisha lengo la mwandishi na kulifanikisha.

**Takriri**: hii ni mbinu ya kurudia rudia maneno na lengo la kupata umbo moja. Katika riway hii ya utengano, mwandishi alitumia mbinu hii kwa kurudia rudia sauti/ sirabi , maneno na pia vifungu vya maneno. Kwa mfano; mimiiiii (UK 47), si kosa lako,………..(UK 48). Takriri kama mbinu hutumiwa kuweka msisitizo wa usemi na pengine kuonyesha yale mambo na hoja ambazo mwandishi hutaka wasomaji wazichunguze kwa ndani ili waibuke na ujumbe aliokusudia.

**Taharuki**: ni mbinu ya kumwacha msomaji na hamu ya kuendelea kujua namna kitu Fulani au tukio Fulani lilivyoisha. Katika riwaya hii ya utengano, mwandishi alitumia taharuki nyingi katika uundaji wa kazi yake. Kwanza kabisa, kuna taharuki pale ambapo, Maksuudi anawafukuza mkewe bi Tamima pamoja na biti kocho na kuwaachisha kitito kile nyumbani. Hatuonyeshi maisha ya kitoto hicho na namna kilivyo fariki. (UK 53 ). Pia, kuna taharuki pale ambapo bi Tamima anafukuzwa nyumbani kwa maksuudi, mwandishi hatuonyeshi mahali anapokwenda na namna mambo yanavyomwendea huko. Taharuki kama mbinu hulenga kuishika hamu ya msomaji ya kuendelea na ile taka/kiu/haja na njaa ya kujua mwisho wa mambo namna ulivyo.

**Majazi**: hii ni mbinu ya kumpa mtu jina ambalo hufanana na tabia au umbile lake. Kwa mfano katika hii riwaya ya utengano, mwandishi ametumia majazi kama; inspekta__kulingana na kazi yake ya kuwa chini ya polisi, kijakazi___kulingana na kazi zake za kike anazozifanya, pumziko__mahali penye raha na starehe nyingi, madongoporomoka___mahali penye nyumba ndogo ndogo zilizo katika hali ya kusitikisha, na mifano mingine mengi.

**Utohozi:** ni mbinu ya kubadilisha matamshi au uandishi wa neno la kigeni ili yalingane na matamshi au uandishi wa lugha ya kienyeji. Kwa mfano, kutohoa kiingereza kwa Kiswahili. Katika riwaya hii ya utengano kuna maneno mengi yaliyotoholewa kutoka lugha ya kiingereza kwelekea lugha ya Kiswahili. Na ni kama yafuatayo; inspekta (uk 70), dereva, hoteli, na kadhalika.

**Chuku:** ni mbinu ya kuongeza chumvi katika habari yoyote ile itolewayo ili iwavutie wasomaji. Pengine, baadhi ya wataalamu huifafanua mbinu hii kama mbinu ya uongo, Pale ambapo mwandishi huzidisha maana ya kitu kadri ya kuwadanganya wasomaji. Katika

riwaya hii, mwandishi alitumia mbinu hii wakati anapofafanua hali yake Mussa mvunguni wakati babake anaingia na kuanza kusemezana na kazija. (uk 12) Pengine amuweka chuku pale anapofafanua kucharazwa kwake bi Tamima na wakati anapoomba msamaha.

**Maswali ya balagha:** hii ni mbinu ya kuuliza maswali yasiyohitaji majibu kwa nia ya kusisitiza. Mwandishi wa riwaya hii ya utengano, ailtumia mbinu hii katika kazi yake. Kwa mfano maswali anayojiuliza maksuudi baada ya mambo kumwendea vibaya na kupatikana kwa mabadiliko, lusu! Nani lusu? (UK 101)

Na mbinu nyingine ambazo hatukuzizungumzia hapa. Ni bora kujikumbusha kuwa huu ni mwongozo na haubebi kila kitu namna kinavyojitokeza katika riwaya nzima. Unakusudia kukusaidia kuichambua riwaya ya utengano tu na kuielewa vizuri. Kwa hivyo inakubidi wewe kama mtumiaji wa mwongozo huu, kuisoma riwaya na kupata mbinu nyingine ambazo zimebakia bila kuangaliwa ili kuipanua na kuikuza Nyanja ya elimu.